ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Yahya Khamis Hamad **Kaimu Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Tatu – Tarehe 20 Januari, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaanza shughuli yetu, naona wananchi wetu na taasisi mbali mbali kwa jumla, zimekuwa na hamu kubwa ya kuja kututembelea katika kuona shughuli zetu na kutusalimu hasa katika kipindi hiki cha mwaka mpya wa 2012.

Kwa hivyo, na leo tunao wageni wapo pale juu, kabla sijaanza maswali ningependa kuwatambulisha ili na nyinyi muweze kuwapokea na kuwakaribisha katika ukumbi wetu huu.

Kwa hivyo, leo katika ukumbi wetu wa juu kuna wageni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania TCRA na wageni hao ni kama ifuatavyo. Nitawataja na nitawaomba kila ninayemtaja kati ya wageni wetu basi wasimame ili Waheshimiwa Wajumbe waweze kuwaona.

Kwanza yupo ndugu yetu Habbi Gunze huyu ni Mkurugenzi wa Masuala ya Utangazaji, tunamkaribisha. Amefuatana na wenzake Bi Elizabeth Nzagi, huyu ni Mkurugenzi wa Sheria na Leseni na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi, tunamkaribisha. Vile vile wengine aliofuatana nao ni Bwana Ennocent Mungy, huyu ni Meneja wa Mawasiliano. Wameambatana pamoja na Maofisa wa Tume ya Utangazaji Zanzibar (ZBC). Tunaomba kuwatambulisha kwenu hawa wageni. Kwa hivyo, hawa waliofuatana na Maofisa kama wapo nao tunawaomba wasimame.

Wageni wetu karibuni sana, katika ukumbi wetu huu asubuhi ya leo na Waheshimiwa Wajumbe wamefurahi kuwaona kwamba mpo hapa, maana yake ni kuwa mnajali shughuli zetu zinazoendelea katika ukumbi huu karibuni sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi zake Uwezo wake na Mambo mengine yanayotokana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mswada wa sheria ya Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Kuhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 42

Kuuzwa kwa Majengo ya Serikali

Mhe. Fatma Mbarouk Said (Kny: Hamza Hassan Juma) – Aliuliza :-

(a) Je, Mhe. Waziri ni kweli kwamba jengo la Makao Makuu ya zamani ya Wizara ya Elimu limeuzwa.

(b) Kama limeuzwa je ameuziwa nani au Kampuni gani na kwa madhumuni gani.

(c) Hivi serikali yetu ina majengo mengi sana kiasi kwamba mengine inabidi yauzwe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu :-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na kwa ridhaa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, jengo lililokuwa Makao Makuu ya Wizara ya Elimu lililopo Shangani mjini Zanzibar, ni jengo la zamani ambalo limejengwa kwa kutumia mali ghafi ya mawe na chokaa. Kutokana na uchakavu mkubwa wa jengo hilo, serikali mnamo mwaka 2010 imeamua kuliuza. Hivyo ni kweli jengo hilo limeuzwa.

b) Mhe. Spika, jengo hilo limeuzwa kwa Nd. Said Salim Awadh, raia wa Tanzania, kwa lengo la kuliendeleza na baadae kulitumia kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

c) Mhe. Spika, serikali inapofanya maamuzi ya kuuza mali au majengo yake haina maana kwamba serikali ina mali au majengo mengi. Serikali inauza majengo yake kutokana na uchakavu na sio kwa sababu nyenginezo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kwa asubuhi ya leo kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c).

(a) Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba jengo hilo limeuzwa mwaka 2010, lakini namuomba atupe tarehe kamili ya mauzo ya jengo hilo.

(b) Nikiwa mjumbe mmoja wapo wa Kamati ya Fedha na Uchumi katika kipindi hicho, tulipewa taarifa rasmi na wizara yake ya Fedha na Uchumi kwa wakati huo, kwamba serikali imezuwia kuuza chochote mpaka baada ya uchaguzi. Je, mauzo hayo yalitokana na amri gani, wakati serikali ilizuwia mauzo ya nyumba za kawaida tu ndogo za wananchi mpaka upite uchaguzi, halafu ikaamua kuuza jengo kama hili katika kipindi hicho hicho, ruhusa hii ilitoka wapi.

(c) Tenda hiyo ilitangazwa na nani na nani na nani walipita katika tenda hiyo, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:

(a) Mhe. Spika, Jengo limeuzwa Oktoba mwaka 2010.

(b) Mhe. Spika, ni kweli serikali imesema kwamba haitauza majengo yake mpaka baada ya ukaguzi, jengo hili lilifanyiwa ukaguzi baadae na kutokana na hali yake serikali iliamua kuliuza.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, katika swali langu sikusema neno ‘ukaguzi’, nilisema neno ‘uchaguzi’.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Nilimsikia ukaguzi. Mhe. Spika, jengo hili lilifanyiwa ukaguzi na serikali tayari ilikuwa imeshafanya maamuzi ya kuliuza jengo hili. Kwa hivyo, liliuzwa kwa amri ya serikali.

(c) Mhe. Spika, kuna taratibu tatu za kuuza mali ya serikali. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi, wanisikilize kwa makini ambapo zote zimo ndani ya sheria yetu ya uuzaji au uhaulishaji wa mali za serikali.

Taratibu ya kwanza ni kuitangaza kwa kupitia tenda. Unaruhusu watu wawasilishe tenda zao, halafu baadae nazifungua na kuangalia yule aliyeshinda nampa.

Taratibu ya pili ni kutangaza kwa njia ya mnada. Taratibu ya tatu ni kwamba mtu mwenyewe anaweza kuomba kuuziwa mali ya serikali na serikali ikiridhika na ikiona kwamba ile bei aliyotoa ni kubwa kuliko *valuation* ambayo mmefanya, basi serikali inaweza ikamuuzia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa watu waliouona waraka wa serikali ambao ulizuwia uuzaji wa majengo ya serikali hadi baada ya uchaguzi. Kwa kuwa yapo maeneo mengi ya serikali ambayo yameuzwa hata baada ya amri hiyo ya serikali. Ni siku mbili tu kabla ya uchaguzi majengo yameuzwa na mengine siku ile ya mwisho ndio majengo yanauzwa.

(a) Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya watendaji na baadhi ya viongozi kutumia msitu huo wa wakati wa uchaguzi kuuza mali kiholela.

(b) Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atuambie jengo hilo limeuzwa kwa thamani gani na zikowapi

(c)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika kwanza nataka niseme ndani ya serikali hii hakuna mtendaji hata mmoja mwenye mamlaka ya kuuza majengo ya serikali.

(a) Majengo ya serikali yanauzwa kwa idhini ya serikali na serikali ni Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, nataka niseme kwamba kama kuna majengo yameuzwa, basi serikali ndio iliyotoa idhini kwamba majengo hayo yauzwe.

(b) Pili, alitaka kujua thamani ya jengo hilo. Jengo hilo tumeliuza kwa 1.5 bilion. Fedha hizo tumeziweka katika mfuko wetu wa kujenga majengo mengine ya serikali. Fedha hizo zitatumika kwa kujenga majengo mapya ya serikali. Sasa hivi Mhe. Spika, jengo la katiba litaanza kujengwa wakati wowote na majengo mengine

yatafuatia. Tumeamua kwa makusudi, majengo yetu yote ya serikali tutakayoyauza fedha zake tutaziweka katika mfuko wa kujenga majengo mengine mapya.

Nam. 73

Suala la Pencheni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza :-

Mtumishi wa Serikali anapomaliza muda wake wa utumishi anastahili kulipwa pencheni yake kwa wakati ili aweze kujikimu kimaisha.

Je, ni utaratibu gani unaotumika kuwalipa watumishi wa serikali kwa wakati pale wanapostaafu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na kwa ridhaa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 73 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu unaotumika kuwalipa watumishi wa Umma kwa wakati pale wanapostaafu ni kama ifuatavyo:-

(i) Mara mtumishi anapostaafu, Wizara yake hupaswa kujaza fomu kwa ajili ya malipo ya kiinua mgongo na pensheni.

(ii) Fomu hizo huwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali mara zinapokamilika kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi wa kina.

(iii) Baada ya ukaguzi na masahihisho kukamilika, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali huwasilisha fomu hizo HAZINA kwa hatua za malipo.

(iv) Malipo ya pensheni na kiinua mgongo hutakiwa kulipwa mara moja tu HAZINA watakapopokea fomu na kuridhika na hesabu hizo. Hata hivyo, baadhi ya nyakati kiinua mgongo huweza kuchelewa kulipwa kutokana na upatikanaji wa fedha, lakini pensheni hulipwa kila mwezi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:

(a) Uzoefu Mhe. Waziri unaonesha watu wanachelewa kulipwa mpaka kukata tamaa na kusababisha kula sikukuu mbili kwa wakati mmoja, ikiwemo Iddi El Fitry

na Iddi El Hajji. Hasa kwa wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, pamoja na wastaafu wanaofanya kazi katika Serikali ya Muungano.

(b) Kwa kuwa fedha hizo zinapitia benki ya PBZ, inakuwaje fedha hizo hazifiki kwa muda muafaka kuzingatia familia za wastaafu kula sikukuu hizo au kusherehekea skukuu hizo kwa dhiki.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naomba niseme kabla ya kujibu maswali ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Jeshi la Wananchi na watumishi wa Muungano, hawa hawahusiani na. Mimi nahusika zaidi na watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini namuelewa, namuelewa ndugu yangu Jaku kwa nini kaniuliza swali hilo, kwa sababu nilikuwa Naibu Waziri wa Fedha kule Tanzania Bara. Naomba tu kwa idhini yako nimsaidie kumpa ufafanuzi.

(a) Mhe. Spika, taratibu za Jeshi Mhe. Spika, zinaanzia toka kwenye kikosi chake, inatoka pale inakwenda mpaka kwenye *brigade* yake kabla haijafika makao makuu. Kwa hivyo, kuna mlolongo kidogo mrefu. Kutokana na hali hiyo kwa wenzetu Tanzania Bara wamerekebisha sheria yao. Hivi sasa wameanzisha utaratibu kwamba miezi sita kabla ya kustaafu zile taratibu zako zianze ili fedha zako zisiweze kuchelewa. Kwa hivyo, naamini sasa hivi kwa utaratibu waliojiwekea, fedha zao zitakuwa zinatoka kwa wakati.

(b) Swali lake la pili amezungumzia kupitia PBZ, sasa sikumfahamu hapo, kiinua mgongo na kupitia PBZ. Kwa sababu unapopata taarifa kwamba mfanyakazi huyu ameshastaafu. Hazina wanachotakiwa kufanya ni kutayarisha *cheque* yake ya kiinua mgongo, ile *cheque* tena haipitii PBZ, unakabidhiwa mwenyewe. Sasa wewe mwenyewe siku unapotaka kwenda kui- *cash*, ukitaka kui- *cash* leo, au ukitaka kui-*cash* kesho, lakini katika kipindi cha miezi sita vyenginevyo ikizidi itabidi ile *cheque* itakuwa imemaliza muda wake mpaka ukatengenezewe nyengine. Kwa hivyo, hizi fedha huwa hazipitii PBZ, isipokuwa wewe mwenyewe ndio unakabidhiwa *cheque* na wewe mwenyewe ndio unaipeleka PBZ kwenda ku-*cash*.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa kumejaa manung'uniko mengi ya wastaafu

kwamba yale mafao yao ya kiinua mgongo baada ya kustaafu yanakuwa na kasoro, na huwa kuna madai mengi, madai ambayo hata sisi wawakilishi huwa yanatukumba mara kwa mara. Anakuja mtu na kusema, nataka niulizie nimedhulumiwa. Je, Mhe. Waziri haoni kuwa kuna haja sasa ya kuweka wazi zaidi ile fomula inayotumika katika kumlipa mtu mafao yake ya kiinua mgongo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, nataka nithubutu kusema kwamba fomula iko wazi kabisa. Fomula iko wazi ndani ya sheria ya kiinua mgongo na kama Mhe. Mjumbe ataihitajia niko tayari kumletea, nitamletea ili na yeye awe nayo na aijuwe. Fomula hii haikatazi mtumishi yeyote kuweza kujua.

Lakini nataka niongeze tu kwamba pale ambapo inatokea mtumishi akalalamika kwamba madai yake labda yamepungua au hivi na hivi. Sisi ndio wafanyakazi, sisi ndio watumishi, kuna baadhi ya wakati tunakuwa na mikopo. Sasa kiinua mgongo chako lazima kimalize ile mikopo ambayo unadaiwa na serikali, sasa huwa tunasahau. Mimi nimeona kwa uzoefu wangu kule Tanzania Bara nilipokuwepo, watumishi wengine walikuwa wanasahau kwamba amekopa friji miaka minane au kumi iliyopita, lile deni halijamalizika. Mimi nilikopeshwa vespa hapa ikachukua miaka 5 hapa nakatwa kidogo kidogo, ningestaafu katikati ingebidi kile kilichobakia kiweze kutolewa. Sasa tunakuwa tunasahau, lakini ukweli ni kwamba mtumishi yeyote yule kama anaona kwamba amedhulumiwa, basi ana haki ya kutoa maelezo yake kwa maandishi ili iweze kuangaliwa tena hesabu zake.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na uzima kwa asubuhi ya leo. Katika majibu mama ya Mhe. Waziri alisema kwamba yeye hawezi kujibu swali hili la Muungano, swali langu liko hapa.

(a) Je, hivi baadhi ya vikosi tunavyoelewa sisi ni vya Muungano. Je, vikosi hivi vinafanyakazi upande mmoja tu.

(b) Ni nani hasa ambaye masuala ya Muungano anayajibu humu katika Baraza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, unapozungumzia masuala ya Muungano, na suala la msingi lilikuwa ni kwa watumishi wetu sisi, ndio pale niliposema siwezi kujibu masuala ya Muungano, lakini nikajaribu kumsaidia Mhe. Mwakilishi kwa sababu naelewa a b c d ya ule utaratibu wa kule kwa wenzetu, ndio dhamira yangu.

Lakini linapokuja suala ndani ya Baraza linalohusiana na Muungano, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio wenye dhamana ya kujibu masuala ya Muungano. Tunasaidiana, kwa sababu yanaweza kuwa ni masuala ya fedha ya Muungano, tunasaidiana na waziri mwenzetu ili kumpa taarifa ambazo sisi tunazielewa, lakini wenye dhamana ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Nam. 51

Nafasi za Watu Wenye Ulemavu Katika Ajira Zanzibar

Mhe. Hamza Hassa Juma – Aliuliza:-

Serikali imepitisha Sera ya Watu Wenye Ulemavu hapa Zanzibar. Miongoni mwa yaliyomo katika sera hiyo ni kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapatiwa huduma zote muhimu za kijamii ikiwemo ajira.

(a) Serikali imetoa kibali kwa baadhi ya wizara kuajiri ili kujaza mapengo, Je, watu wenye ulemavu wamezingatiwa kwa kiasi gani.

(b) Katika kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu, je kuna orodha au faili yoyote iliyotengwa kwa ajili ya kuwatambua.

(c) Je, katika kipindi hiki cha mwaka mmoja watu wangapi wenye ulemavu wamepatiwa ajira.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 51 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba miongoni mwa mambo yaliomo katika sera ya watu wenye ulemavu ni pamoja na kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapatiwa huduma zote muhimu za kijamii ikiwemo ajira.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo.

(a) Ni kweli serikali imetoa kibali cha kuajiri kwa baadhi ya wizara ili kujaza mapengo mbali mbali. Hata hivyo, vibali vilivyotolewa havikutofautisha baina ya waombaji wa kazi kwa watu wenye

ulemavu na wasiokuwa walemavu. Hali hii inatokana na ukweli kwamba wizara yangu ilipokuwa ikipokea maombi ya kazi haikuwa ikitenga mambi ya watu wenye ulemavu na wasiokuwa walemavu, kwa maana hiyo waombaji wote walizingatiwa kwa usawa.

(b) Kama nilivyotangulia kujibu sehemu (a) ya swali hili, haukuwa na jalada maalum la maombi ya kazi kwa watu wenye ulemavu, utaratibu ambao ulipelekea uchaguzi wa kijumla wa waombaji kazi.

(c) Kama nilivyotangulia kujibu swali kwenye sehemu (a) na (b), wizara yangu haikuwa ikitafautisha baina ya watu wenye ulemavu na wasiokuwa na ulemavu. Hivyo kwa sasa ni vigumu kueleza ni watu wangapi wenye ulemavu walioajiriwa, kwa vile taratibu zilizokuwepo hazikuwa zikilazimisha kutenganisha baina ya watu wenye ulemavu na wasiokuwa walemavu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii tena ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini bado kwa kuwa wizara yake ndio inayoshughulika na masuala ya utumishi wa umma, na kwa kuwa chombo hiki hiki cha wananchi ndio kilichotunga hizo sera na ikazipitisha na kuziidhinisha, ili wenzetu wenye ulemavu waweze na wao kupata haki ya ajira, hasa ukizingatia kwamba wao ni tofauti na wale wengine waliokamilika viungo vyao au miili yao. Swali langu liko hapa.

Mhe. Spika, kwa kuwa baada ya kufanya utafiti mimi mwenyewe nimegundua kwamba katika hii ajira ya muda ya kujaza mapengo hatukuwaona walemavu ambao wameajiriwa. Kwa kuwa kuwa idara ya watu wenye ulemavu. Je, Mhe. Waziri haoni sasa hivi kuna haja ya kuwaandikia idara ya watu wenye ulemavu ili kupeleka orodha ya wale watu wenye ulemavu wenye sifa za kuweza kuajiriwa serikalini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na yeye kwamba chombo hiki ndicho kinachotunga sheria na serikali ndio inayotunga sera, lakini usimamizi wa shughuli zote hizo za utekelezaji wa sheria na sera chombo hiki ndicho ambacho kinazifuatilia.

Kuhusu suala la kuweka utaratibu kama nilivyosema kwenye suala langu la juzi kwamba tayari wizara ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, imo katika mchakato wa kutengeneza orodha ya kuwatambua walemavu wote ambao wana ujuzi na wanastahiki kupata ajira serikalini.

Mhe. Spika, katika sheria ya utumishi wa umma kufuatia utaratibu wa uwajiri serikalini ni kwamba mtu yeyote mwenye sifa, wakiwemo ndugu zetu wenye ulemavu nadhani ni watu ambao wataajiriwa kwa mujibu wa sifa zao. Lakini pale ambapo nafasi za ajira zilizopo ni chache, lakini wamejitokeza ndugu zetu watu wenye ulemavu, ndio pale Katibu Mkuu Kiongozi alipopewa nafasi ya kutoa ahuweni kwa watu wetu wenye ulemavu. Kwa hivyo, nataka nimuhakikishie Mhe. Hamza Hassan kwamba jambo hilo lipo.

Mhe. Spika, lakini katika vibali vilivyotolewa vilitolewa katika maeneo maalum kwa wataalamu maalum ambao waliokuwepo kwa wakati huo. Kwa kweli siwezi kusema kwa bahati nzuri, lakini kwa bahati mbaya ndugu zetu Watu Wenyeulemavu katika hivyo vibali vilivyotolewa hawakuwemo na wala hawakujitokeza.

Nam. 54

Ushiriki wa Wazanzibari Baraza la Mitihani la Taifa

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Elimu ya juu ni ya Muungano.

(a) Kuna ushiriki gani kwa Wazanzibari katika vyombo vya Elimu ya Juu kama vile Baraza la Mitihani la Taifa?

(b) Kwa kudhihirisha kwamba kweli tunafanya kazi zetu kwa pamoja ni mwaka gani ambao Baraza la Mitihani la Taifa limepanga usahihishaji wa mitihani kufanyika hapa Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, wakati nanyanyuka kuja kujibu nimeulizwa leo unakwenda mwenyewe? Kweli leo nimekuja mwenyewe kwa sababu Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali macho yake kidogo yanamsumbua, kwa hivyo ni vyema apumzike.

Mhe. Spika, kwa idhini yako kwanza napenda kutoa utangulizi kabla kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kwa Elimu ya Juu ni suala la Muungano na Wajumbe kutoka Zanzibar wanashirikishwa katika Vyombo vinavyosimamia Elimu ya Juu kama vile Baraza la Mitihani la Taifa, Kamishna ya Elimu Tanzania (*TCU*) na Bodi ya Mikopo.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawakilishwa katika vyombo mbali mbali vya Elimu ya Juu vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mfano, katika Bodi ya Baraza la Mitihani ya Tanzania wapo wajumbe wanne wa Zanzibar, pia wapo wajumbe wanne wanaowakilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Kamisheni ya Elimu Tanzania (*TCU*). Aidha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inao wajumbe wawili katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania.

(b) Baraza la Mitihani Tanzania hivi sasa limejenga Kituo Maalum cha Usahihishaji wa Mitihani huko Dar-es-Salaam kwa lengo la kuhakikisha kuwa mitihani yote inasahihishwa katika kituo kimoja tu badala ya mitihani kusahihishwa kwenye maeneo mbali mbali. Kwa kufanya hivyo, usimamizi wa kazi usahihishaji wa mitihani unakuwa wa ufanisi zaidi na unapunguza gharama.

Kwa vile Baraza la Mitihani ni chombo cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Serikali ya Muungano wa Tanzania, wizara yangu haijapata habari kwamba Baraza la Mitihani la Tanzania linakusudia kuweka kituo cha usahihishaji wa mitihani hapa Zanzibar mpaka hivi sasa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Serikali ya Muungano wa Tanzania sehemu ya Idara ya Elimu ya Juu kuna nafasi ya *Principal Education Officer*. Kwa kweli nafasi hii mara nyingi mtu kutoka Zanzibar ndiye anayeiwakilisha pale. Lakini tokea mwaka 2010 *officer* ambaye aliyekuwa akishikilia nafasi ile amestaafu hadi hii leo nafasi ile bado haijajazwa.

(a) Je, Mhe. Waziri nafasi hii hakuna Mzanzibari mwenye sifa ya kwenda kujaza ile nafasi, pia huoni Zanzibar inakosa nafasi yake ya uwakilishi katika taasisi ile?

(b) Katika *Desk* la *UNESCO* kuna nafasi ya Mkurugenzi Msaidizi na mara nyingi nafasi hii anakuwa na Mzanzibari. Je, suala hili ni kweli na kama ni kweli ni Mzanzibari gani anayewakilisha nafasi hiyo kwa sasa?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli hiyo nafasi aliyoitaja mwanzo alikuwepo Mzanzibari ambaye alikuwa akiwakilisha Zanzibar katika sehemu hiyo. Mzanzibari yule alifika umri wa kustaafu, kwa hivyo ikambidi astaafu.

Hata hivyo, wenzetu wakatuahidi kwamba yule Mzanzibari watamchukua tena kwa mkataba, lakini kwa bahati mbaya walipoomba Idara ya Utumishi Serikali walikataa kutoa mkataba.

Sasa katika mazungumzo yetu ya juzi na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Serikali ya Muungano wa Tanzania tulikubaliana kwamba nafasi hizi hivi sasa bora zijazwe. Kwa hivyo, tayari tumeshatengeneza majina na tumeshawasilisha, ili wajaze nafasi ile.

Katika *UNESCO* pia tumekubaliana kwamba nafasi hii sasa ijazwe na wamekubali. Kwa hivyo, hivi sasa tuko katika jitihada za kujaza nafasi hiyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa faida ya Baraza lako kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutueleza kwamba Bodi ya Elimu ya Juu inawakilishwa na wajumbe wanne kutoka Zanzibar na Bodi ya Mikopo ina Wajumbe wawili kutoka Zanzibar.

Sasa kwa faida ya Baraza lako pamoja na kujua uwiano wa hicho chombo, kwa sababu ni chombo cha Muungano, basi namuomba Mhe. Waziri atueleze kwamba Bodi ya Elimu ya Juu ina wajumbe wangapi na ile Bodi ya Mikopo ina wajumbe wangapi, yaani idadi ya wajumbe wote, ili tupate kujua uwiano unakwenda sawa?

Pili amesema kuwa mpaka hivi sasa hakuna mpango au haijawekwa siku ya kusahihishwa mitihani kwa upande wa Zanzibar na wakati chombo hiki ni cha Muungano. Je, haoni kutofanya hivyo ni kuinyima haki Zanzibar, kwa hiyo na sisi tunahitaji Zanzibar mitihani isahihishwe kwa upande wa Zanzibar, hivyo ni lini hasa Zanzibar itapata fursa hii?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, katika *TCU* jumla ya wajumbe 22 na sisi tunao wanne. Katika Baraza la Mitihani jumla ya wajumbe ni 12 na sisi tunao wanne. Vile vile katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu jumla ya wajumbe ni 13 na sisi tunao wawili. *(Makofi)*

Mhe. Mjumbe, amezungumzia kuhusu suala la uwiano. Kwa kweli sikatai suala la uwiano, lakini nasema ni kitu muhimu ni *competence* ya mjumbe katika kile chombo anapokuwa anawakilisha. Kwa mfano, kama atakuwa anafanyakazi yake vizuri, maana vyombo hivi haviamui kwa kura, isipokuwa vinaamua kwa hoja na *consensus*. Kwa hivyo, kama atafanyakazi yake vizuri na *consensus* ikapatikana upande wake, basi hiyo nafasi ya kuitetea Zanzibar inapatikana bila ya tatizo lolote.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba tufike mahala kwamba tuwe sawa kwa sawa Zanzibar na Tanzania Bara. Lakini kwa hivi sasa bado nasema hakujana na tatizo, isipokuwa jambo muhimu ni yule mjumbe kuwa madhubuti katika kuwakilisha zile hoja zake kwa manufaa ya Zanzibar.

Kuhusu suala la kusahihisha Mhe. Spika, dunia tunayoishi hivi sasa ni tofauti na kule tunakotoka. Kwa kweli hivi sasa suala la kusahihisha lazima linatakiwa liwe linafanyiwa *monitoring* nzuri sana.

Kwa mfano, kuna wizara moja Mhe. Spika, waliingia watu kwenda kuiba *computer* na walikuwa wawili, basi mmoja alinyanyua *computer* na kumpa mwenziwe akapokea na baadaye wakatoka na kwenda zao.

Sasa wakati ilipokuja kubainika kwamba ile *computer* imeibiwa na shaka akatiliwa yule mwizi basi alikataa sana. Mhe. Spika, kwa technology za kisasa alioneshwa picha yake namna alivyoichukua *computer* na kumpa yule mwenziwe na sura ni yake.

Mhe. Spika, katika kusahihisha mitihani hivi sasa inawezekana mtu akawa anafanya majungu pale juu ya meza yake, basi lazima kuwe na *monitoring* nzuri ambayo inamuangalia yule mtu, ili likitokea tatizo aweze kupatikana kwa ushahidi kamili. Kutokana na hali hiyo, ndio maana hawa wenzetu wakajenga Kituo Maalum cha Kusahihisha Mitihani.

Nam. 72

Ahadi za Rais

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anapokuwa katika ziara zake za kutembelea wananchi na kukagua au kufungua miradi ya maendeleoo huwa anakutana na majukumu ya papo kwa papo kuyatolea ahadi, ili yapate kutekelezwa.

(a) Je, ni wizara au idara gani inayoratibu utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais?

(b) Je, inafuatilia utekelezaji kwa ukamilifu wa ahadi hizo?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Mjumbe kwa ufuatiliaji wake mzuri wa mambo yanayohusu jimbo lake hasa hizi ahadi za Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa akiwemo Mhe. Rais. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Wizara zinazoratibu utekelezaji wa ahadi za papo kwa papo zinazotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati anapokuwa katika ziara zake za kutembelea wananchi na kukagua au kufungua miradi ya maendeleo ni Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambayo ndio Ofisi inayoratibu utekelezaji wa shughuli za serikali. Aidha ahadi hizo huwa zinatekelezwa na sekta husika.

(b) Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais huwa wanafuatilia ahadi zote zinazotolewa na Mhe. Rais na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kwa manufaa ya wananchi kwa eneo ilipotolewa ahadi na kwa taifa kwa ujumla.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ni muafaka kabisa.

Mhe. Waziri miongoni mwa ahadi ambazo bado hazijatekelezwa mpaka muda huu, kuna ajali ambayo ilitokezea kipindi cha Uchaguzi mwaka 2010 kuna mwananchi mmoja Jambiani alipoteza mkono wake anaitwa Pandu Mkasi Juma.

(a) Je, kuna kauli gani kwa Mhe. Rais kuhusu kusaidiwa mkono wake wa bandia?

(b) Miongoni mwa ahadi zilizotolewa na Rais Mstaafu Kamati ilitembelea Skuli ya Kengeja na iliahidiwa *computer* na Rais Mstaafu hadi leo bado hawajapata computer hizo ikiwemo na Skuli ya Mwambe. Je, kuna kauli gani kuhusu suala hilo?*(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakiri kuwepo kwa ahadi hizi. Lakini tatizo ni kwamba ahadi hizi ni nyingi na inabidi tuzifanye kwa nyakati tofauti.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe kwamba tukitoka hapa mimi na yeye tukae pamoja na nitazichukua ahadi hizi tutazifuatilia ofisi yangu kwa ajili ya kuzikamilisha. *(Makofi)*

Mhe. Amina Idd Mabrouk: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Rais anapofanya ziara zake huwa anafuatana na Mawaziri. Vile vile Mhe. Rais anapotoa ahadi zake kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba ahadi anazotoa huwa zinafuatiliwa na wizara husika.

Je, Waheshimiwa Mawaziri wanapotoa ahadi zao zinafuatiliwa na nani?

Vile vile ahadi zile wanazotoa Waheshimiwa Mawaziri bado hawajazitekeleza na wanaendelea kudaiwa pamoja na kuandikiwa barua.

Je, Mhe. Waziri atalieleza nini Baraza hili kuhusu suala la mawaziri?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, swali la msingi lilikuwa ni kuhusu ahadi za Mhe. Rais. Sasa kama ahadi za Mhe. Waziri usione tabu mfuate tena mkumbushe kwa ajili ya kuzimaliza, kwa sababu sote ni wawakilishi, basi ni vyema kukumbusha kwa ajili ya kufanyakazi kwa pamoja, yaani wewe mwakilishi wa jimbo na yule waziri mwenye sekta, mkumbushe mlimalize.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa lengo la serikali yetu ni kuwaweka Marais wetu katika mazingira mazuri hasa pale wanapostaafu. Vile vile Marais wetu wakati wanapostaafu tayari huwa kuna ahadi wameshaweka, ambazo bado hawajazitekeleza.

Je, ni lini serikali itawaweka katika mazingira mazuri Marais wetu Wastaafu kwa kutekeleza ahadi walizoziweka kama vile ujenzi wa hospitali iliopo Kikunguni katika Jimbo la Wawi? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza tunamshukuru sana Mhe. Mjumbe kwa kweli wewe tumekupa jina Kingunge kwa ukereketwa wako kwa kufuatilia mambo, tena hongera sana na endelea hivyo. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, kuhusu hizi ahadi za Waheshimiwa Marais Wastaafu kama nilivyosema tatizo ni muda tu wa utekelezaji, kwa sababu ahadi ni nyingi. Kwa hivyo, napenda kusema kwamba sisi tutaziratibu, lakini kama unazikumbuka zipo, basi usione tabu nikumbushe, tutazifanyia mpango kwa ajili ya kuzitekeleza mara moja.

Nam. 11

Usajili wa Vyama vya Ushirika

Mhe. Salma Mussa Bilali – Aliuliza:-

Kwa kuwa Idara ya Ushirika inaendelea kusajili vyama idadi kubwa ya Vyama vya Ushirika vilivyosambaa katika Wilaya zetu za Unguja na Pemba na kwa kuwa vyama vyote hivyo vinahitaji ulezi na usimamizi wa karibu wa maafisa ushirika, ambapo kwa sasa yupo mmoja tu kwa kila wilaya. Vile vile kwa kuwa vyama hivyo ni vingi kuliko uwezo wa afisa mmoja.

Je, wizara itakubaliana na mimi kuwa ipo haja ya kuongeza idadi ya maafisa ushirika, ili angalau Afisa Ushirika mmoja kila jimbo, kwa ajili ya kukabiliana na wingi wa vyama vinavyoendelea kuongezeka kila siku.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 kama hivi ifuatavyo:-

Nakubaliana naye Mhe. Mjumbe kwamba kweli kumekuwa na ongezeko la uandikishaji wa Vyama vya Ushirika. Vile vile nakubaliana naye kuwa kumekuwa na tatizo la kupata wataalamu wa kuvisimamia vyama hivyo. Hivi sasa wizara yangu inakusudia kupanga mikakati maalum ya kutoa mafunzo maalum kwa wale waliopo, lakini pia kutafuta wengine ambao watakuwa na uwezo na taaluma ya kutosha katika kusimamia Vyama vya Ushirika.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri. Kwa kweli kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi kuhusu ucheleweshwaji wa usajili wa Vyama vyao vya Ushirika wakati wakapohitaji usajili katika idara yako na kufikia hadi kukata tamaa ya kupata Hati zao za Usajili. Kwa hivyo, ni sababu zipi ambazo zinasababisha hali hii?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, malalamiko hayo na mimi nimekuwa nikiyasikia pia. Kwa kweli kumekuwa na tatizo, lakini tatizo la kimsingi ndio kama lile ambalo nimeeleza jana katika swali mama, kwamba kila mtu anaanzisha Chama chake cha Ushirika kwa vile anavyohisi yeye ndivyo.

Sasa utaratibu wetu huwezi kuanzisha chama kama hatujakikagua, hapo ndipo panapoonekana panachukua muda mrefu. Kwa kweli huwezi kuanzisha chama tu, kwa sababu unataka kuwakusanya vijana au wananchi wako ukasema kwamba hiki kitakuwa Chama cha Ushirika, isipokuwa kuna taratibu zake za kuzifuata, sasa kama zile taratibu hazikufuatwa inabidi tufuatilie.

Kwa hivyo, hivi sasa tunajitahidi na ule ucheleweshaji uliokuwa ukifanyika huko nyuma sasa kwa kiasi kikubwa tumepiga hatua nzuri.

Mhe. Spika, tutaendelea kujitahidi *speed* ya kuvisajili pamoja na kuvifuatilia vyama vyetu tutaongeza, lakini tatizo ndio lile ambalo alilisema Mhe. Mjumbe ni kuwa hatuna maafisa wa kutosha katika wilaya zetu kwa ajili ya kutusaidia.

Kutokana na hali hiyo, suala la msingi ni kutafuta wasaidizi wetu huko wilayani, ili baadaye tuweze kusajili kwa uhakika tena kwa haraka zaidi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Kwa kuwa *concept* ya Vyama vya Ushirika ni kutoa ajira zaidi kwa wananchi wetu. Lakini kwa kuwa Vyama vingi vya Ushirika vilivyoanzishwa vinakuwa havipati maendeleo mazuri kutokana na taaluma ndogo ya kuweza kujilea pamoja na kujiendeleza.

Je, wizara yake Mhe. Waziri ina mkakati gani wa kufikiria Chuo cha Ushirika kama ambavyo wenzetu Tanzania Bara wanacho na kinasaidia sana kutoa taaluma ya Vyama vya Ushirika?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, mpaka hivi sasa bado hatujawa na mpango wa kuanzisha Chuo cha Ushirika.

Kwa kweli, hivi sasa tumejipanga katika kila wilaya kuanzisha Vituo Maalum vya *Study* Maalum ikiwemo kuviimarisha Vyama vya Ushirika, *SACCOS* na vyama vyengine ambavyo vinafanya jumuia kama hizo, kwa ajili ya kuwapatia mafunzo katika maeneo yao katika kila wilaya.

Tatizo liliopo ni kwamba tukijenga Chuo cha Ushirika wanaweza kufaidika wale tu ambao wako karibu ya eneo lile.

Kwa hivyo, jambo tunalokusudia kufanya katika kila wilaya ni kujenga Vituo hivyo vya Mafunzo ya *Study* Maalum, ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu kwa ajili ya kupata taalum na hatimaye kupata ajira.

Mhe. Spika, tunakusudia Vyama vya Ushirika vizalishe ajira zaidi ya 3000. Kutokana na mipango ambayo tumeipanga hivi sasa na kwenye bajeti inayokuja, basi ninahakika suala hili tunaweza kupiga hatua kubwa sana ya kuongeza ajira. Ni kweli Vyama vya Ushirika vikiimarika na ajira zinaimarika katika Sekta Binafsi.

Nam. 31

Ufinyu wa Hospitali za Rufaa

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Eneo la Hospitali Kuu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja limekuwa dogo mno. nafasi iliyopo haitoshi kufnaya upanuzi wa hospitali hiyo ikihitajika.

(a) Kwa kuwa Mjini Unguja kwa sasa hakuna eneo la kujenga Hospitali kubwa ya Rufaa na kwa vile iliyopo sasa haitoshi. Wizara ina mpango gani wa kutafuta eneo jengine la kujenga hospitali kwa nafasi?

(b) Ili kuondoa msongomano wa matibabu hospitalini hapo kwa aina mbali mbali za maradhi. Kwa nini serikali haijengi hospitali ya rufaa nyengine ambayo itakuwa maalum kwa baadhi ya maradhi tu, ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Mnazi Mmoja?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 31 kama ifuatavyo. Lakini kwanza napenda kutoa maelezo kabla ya kumjibu swali lake.

Ili kuweza kuanzisha Hospitali ya Rufaa kuna changamoto nyingi inabidi ziangaliwe kabla ya kujengwa hospitali hiyo.

(i) Upatikanaji wa wafanyakazi wa kutosha wa kada mbali mbali;
(ii) Vifaa muhimu na madawa;
(iii) Fedha kwa ajili ya ujenzi huo.

Mhe. Spika, maamuzi ya serikali ya kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe ni ya Rufaa kwa Zanzibar tayari yameshapitishwa. Lakini hospitali hiyo kwa sasa inatumika pia kama ni Hospitali ya Mkoa wa Mjini Magharibi imekuwa ndogo na wala haikidhi haja kwa Mjini Unguja. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ili hospitali hiyo ifanyekazi hiyo ya rufaa, basi kweli

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, samahani kidogo kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, namuomba Mhe. Naibu Waziri aongeze sauti, kwa sababu hatusikii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nitoe maelezo kabla ya kujibu swali la Mhe. Mjumbe Nam. 31 lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kweli kuna changamoto nyingi ambazo inabidi ziangaliwe kabla ya kujengwa Hospitali nyengine ya Rufaa.

- Upatikanaji wa wafanyakazi wa kutosha wa kada mbali mbali;
- Vifaa muhimu na madawa;
- Fedha kwa ajili ya ujenzi huo.

Mhe. Spika, maamuzi ya serikali ya kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe ni ya Rufaa kwa Zanzibar tayari yameshapitishwa. Lakini hospitali hiyo kwa sasa inatumika pia kama ni Hospitali ya Mkoa wa Mjini Magharibi imekuwa ndogo na wala haikidhi haja kwa Mjini Unguja. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ili hospitali hiyo ifanyekazi hiyo ya rufaa, basi kweli kuna haja ya kuwa hospitali nyengine katika eneo la mjini, ambayo itoe huduma kwa ajili ya wananchi wa Mjini Unguja.

Mhe. Spika, kuchanganya huduma za rufaa na huduma nyenginezo za hospitali za kawaida katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ndiko kunakoifanya hospitali hiyo kuwa haitoshi, kwani mbali ya wagonjwa wa mjini bado inabidi ipokee wagonjwa kutoka nchi, yaani Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 31 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wizara imeliona hilo na iko katika mchakato wa kutafuta sehemu ambayo Hospitali ya Mkoa wa Mjini Magharibi itajengwa, ili kupunguza hilo tatizo na Hospitali ya Mnazi Mmoja ibaki kuwa ni Hospitali ya Rufaa.

(b) Mhe. Spika, ni kweli eneo la Hospitali ya Mnazi Mmoja limekuwa halitoshi kwa upanuzi wa huduma nyengine. Lakini katika hatua za kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali hiyo, serikali imeshatiliana mkataba saini na nchi ya Norway, ili kukitumia kilichokuwa Kiwanda cha Madawa ambacho kipo pembezoni mwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa upanuzi wa hospitali hiyo.

Mradi huo utakapokamilika basi baadhi ya huduma zitahama katika majengo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na kuhamia kwenye jengo hilo jipya, ili kuipa nafasi hospitali hiyo kutoa huduma za rufaa katika majengo mengine zaidi.

Wakati huo huo kuimarisha Hospitali za Wilaya na zitapunguza mzigo kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, kwani matibabu mengi yanafanyika au yatafanyika huko wilayani bila ya kuwa na haja ya kuwaleta wagonjwa mjini.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu wa Afya amekiri kwamba eneo lile ni dogo halitoshi kwa upanuzi wa Hospitali ya Rufaa. Lakini kwa kuwa hospitali iliopo haikuzingatia matumizi mazuri ya ardhi kwa kujenga majengo ambayo hayakwenda juu sana na tayari yameshakuwa machakavu.

Je, ni lini serikali itaitumia ardhi ile ya pale Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kujenga majengo ya kisasa na yaliyokwenda juu?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kwamba hospitali haikuzingatia matumizi mazuri ya ardhi kwa kujenga majengo yaliochini. Lakini anapendekeza kuwa ardhi ile itumike kwa kujenga majengo yaliyokwenda juu.

Mhe. Spika, nafikiri hilo si kwa hospitali tu nchi nzima hatukuzingatia hilo kwamba nchi yetu ni ndogo. Lakini mbali na hilo ni kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kama tunataka iwe Rufaa, basi yale yaliopo kama yatahamishwa na kile ambacho tunachotaka kukiongezea pale, nadhani yatatutosha kwa sababu sehemu nyengine ikiwa itafanyakazi kama Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwa hivyo, kilichopo pale ambalo ni jengo la chini ni Msikiti tu, ndilo ninaloliona mimi. Kwa hivyo, kama unataka tuvunje Msikiti kwa idhini yako basi mimi sina tatizo, tutavunja Msikiti na tutafanya mchango na kuweka kufanya utaratibu kwa ajili ya kujenga Msikiti wa ghorofa, kwa sababu watu wanasali pale na wala hatuwezi kuvunja Msikiti bila ya kufanya shughuli nyengine, vyenginevyo jengo la chini jengine silioni pale. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Inaonekana Wizara ya Afya inajenga majengo yake kwa kufuata idhini ya mtu na sio idhini ya Mipango Miji. Je, Mhe. Naibu Waziri atatueleza nini kuhusu ujenzi mpya wa Hospitali ya Mnazi Mmoja utafuata idhini ya mtu fulani badala ya Mipango Miji?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sijafahamu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali lako.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, wakati Mhe. Naibu Waziri wa Afya alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mhe. Saleh Nassor Juma alionesha kuwa alionesha kwamba anahitaji idhini ya Maalim Saleh ndio ajenge majengo ya kwenda juu na sio idhini ya mipango miji.

Namuuliza hata huo upanuzi wa hospitali ya rufaa inaelekea anasubiri matakwa ya mtu fulani badala ya Mipango Miji.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, hospitali ya Mnazi Mmoja ipo katika Mji Mkongwe na tunachokijenga chochote inabidi tuwa *consult* watu wa Mji Mkongwe na watupe ruhusa. Kwa hiyo kinachojengwa pale huwa kinafanyika kwa idhini ya Mji Mkongwe na si vyenginevyo.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ibara ya 58 kifungu kidogo cha (1) ni kwamba kila mjumbe atalisema jambo ambalo lipo katika mjadala tu na hatarudia. Kwa namna yoyote ile maneno yake au maneno yaliyokwisha kusemwa na wajumbe wengine.

Sasa neon lililokuwepo katika mjadala ni kuhusu hospitali. Sikuzungumzia habari ya Msikiti. Nilizungumzia habari ya majengo ya hospitali ni mafupi na kwa hivyo hayakuzingatia mipango miji. Je, ni lini serikali itaweka mpango ambao yale majengo ya hospitali yaliyokuwa mafupi yatapandishwa juu na sikuzungumzia Msikiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumjibu Mheshimiwa na kumsaidia Mhe. Waziri wangu, alichokuwa akieleza Naibu ni kwamba takriban majengo yaliyokuwepo pale mengi ni ya ghorofa, ukiacha lile la msikiti. Hatuwezi kujenga jumba la ghorofa zaidi nadhani Mhe. Hija alijaribu kuliweka sawa bila ya idhini ya Mji Mkongwe.

Kwa hivyo suala lake la kwamba tujenge majengo ya kwenda juu haitawezekana bila ya ruhusa ya Mji Mkongwe yaani Mamlaka ya Mji Mkongwe. Hata hapo tunatotaka kuongeza mradi wa orio, ramani tulizochora ilibadi mpaka tupate idhini ya Mji Mkongwe ndipo tuje tujenge kule kwenye kiwanda ambacho ni cha madawa hivi sasa.

Kwa hivyo nadhani kama hakumfahamu Naibu Wangu basi hilo tunaomba atustahamilie. Lakini dhamiri yake kwamba majengo yaliyokuwepo pale ni ya ghorofa na mimi vile vile pale silioni la chini pale, isipokuwa ghorofa zile ni kwa sababu ya utaratibu wa Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nisaidie kidogo. Wengi tunafikiri kwamba Mji Mkongwe tutaweza kujenga nyumba ya ghorofa kumi. Mji Mkongwe mwisho kwa kwa mujibu wa sheria ni ghorofa tatu si zaidi ya hapo. Ahsante Mheshimiwa.

Nam. 88
Heshima ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Katika miaka ya nyuma heshima ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ilikuwa inaonekana wazi wazi kwa Mahoteli kufungwa wakati wa mchana, lakini hata nidhamu za mavazi na mambo mengine huwa inazidi. Lakini katika Ramadhani

iliyopita tulishuhudia baadhi ya mahoteli kufanya shughuli zake wakati wa mchana, na watu kutojali kwa mambo mengine ya kinidhamu kulionekana kuzidi kiasi ambacho kinatishia mustakabali wa funga zetu kwa siku zijazo.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako haioni kuwa kuna haja ya kuwepo sheria ya kuratibu baadhi ya mambo ya kiindhari kwa ajili ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

(b) Kama haja hiyo ipo, ni lini wananchi wa Zanzibar wategemee kupata sheria hiyo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Anajibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 88 (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli na nakubaliana na Mhe. Mjumbe kuwa nidhamu na mambo mengine kama vile kuwapo kwa mahoteli ya kula mchana katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani imeshuka. Hata kwa ndugu zetu wa kike nao wanapaswa kulaumiwa kwa mavazi yao. Heshima ile iliyokuwepo hapo nyuma kwa kueheshimu Mwezi huu mtukufu wa Ramadhani sasa haipo tena na imepotea kabisa.

Hata hivyo sikubaliani na Mhe. Mwakilishi kwamba haya yanatishia mustakbali wa funga zetu. Funga ni imani na inamtaka mtu yeyote ajifunge kwa ukweli ili moyo wake uweze kustahamili mambo kama hayo.

Mhe. Spika, serikali inakwerwa sana na jambo hili na tayari imeshaanza kulichukulia hatua kwa kuteua Kamati ya Mawaziri ya kulichunguza kwa kina tatizo hili. Kamati hiyo ina waheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kama ni Mwenyekiti, Waziri wa Ustawi wa Jamii, Wanawake, Watoto na Vijana, Mjumbe na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Raisi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia na yeye ni Mjumbe.

Kamati hii tumeshaanza kukutana na pia tumeshapata maoni mengi na mazuri kutoka kwa wadau wengi. Wadao hao ni pamoja na Jumuia ya Maimamu, Mashekhe mbali mbali wa kiume na mshekhe wa kike kwa kupitia jumuia yao, Mufti, Kadhi Mkuu, Katibu Mtendaji wa Wakfu na kadhalika.

Maoni haya sasa tunayafanyia kazi na baadaye tutafikisha mapendekezo yetu serikalini ili serikali iweze kutoa muongozo wake. Naamini baada ya hapo serikali itatoa muongozo wake wa busara kuwa nini tufanye ili kurekebisha matatizo haya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Saydina Abubakar kwa kuwa makini kwa suala hili kwa kuteuwa Kamati au Tume makini, nikupongeze kwa dhati kabisa.

Suala langu nililouliza halijapata jawabu. Nilichouliza je, serikali haiyoni ipo haja au haipo haja. Sijauliza kama serikali inakerwa na suala hili au haikwerwi. Najua kuwa serikali inakerwa na suala hili na imeshachukua hatua kuhusiana na suala hili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nafikiri jibu linaonesha dhahiri kwamba serikali imekerwa na masuala haya. Na kama imekwerwa na suala haya ndio maana ikateuwa Kamati na hii Kamati ikishakumaliza itatoa mapendekezo yake nini tufanye ili turekebishe matatizo haya. Nini tufanye ni pamoja ama tufanye sheria au pengine tunaweza tukasema kwamba sheria tusifanye lakini tufanye mambo haya na haya ili tuweze kulikabili.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Nashukuru kwa kunipatia tena nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa mtandao wa mwili wa binaadamu una vichocheo vingi vinavyoitwa *hormones.* Na kwa kuwa jicho linapoona basi *hormones* hupelekwa kwenye kichwa halafu baadaye wakatolewa *hormones* wengine kupelekwa katika viuongo ambavyo vinaweza vikasababisha saumu ile kuondoka.

(a) Je, kwa kuendelea serikali kuwaachia hawa akina mama wakivaa vimini na viguo vifupi si kuzorotesha hii ibada ya Swaumu.

(b) Kwa kuwa viongozi wetu wa awamu ya mwanzo waliweka *presidential decree* ya kuwapiga mikwaju pale pale waliovaa nguo vupi na nguo zinazobana. Je, isingekuwa vyema kwa ile *presidential decree* ya mwaka 1965 iliyotolewa na marehemu Mzee Abeid Amani Karume ikarejea kusudi kuendeleza ibada katika nchi hii.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi masuala yake mawili kama inavyofuata.

(a) Mimi sikubaliani nae kwamba kuna *hormones* ambazo zinamshawishi mtu kufanya hayo aliyoyasema. Ikiwa *hormones* hizo zipo basi ni kwake yeye tu, lakini kwa sisi hazipo. Mhe. Spika, mimi ni Muislamu mzuri na namzidi kwa umri, na miaka yote hiyo bado sijapata *hormones* namna hiyo. Sasa labda kuwe kuna matatizo mengine.

(b) Kweli kulikuwa kuna *presidential decree* ambayo ilikuwa inafanya hivyo ilivyokuwa inasema lakini hiyo ni 1964 na 1965, tumepitwa na wakati mkubwa hivi sasa. Ndio maana serikali hii ikasema hebu tutizameni yale matatizo yote na tukishakuyapata matatizo yote ndio serikali itajua tufanye nini. Ili kurekebisha huo ubovu uliyopo. Na haya Mhe. Spika, kama nilivyokwambia kamati hii inashughulika na kwa sababu wote katika Kamati hii ni waislamu wazuri tu na wanaokereketwa na Maalhajji wakubwa. Naamini kwamba suala hilo tutalimaliza haraka kabla ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Salim Abdalla Hamadi: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuuliza suali la nyongeza.

Mhe. Spika, kabla sijauliza suali la nyongeza naomba kuunga mkono maneno ya Mhe. Saleh kuwa *hormones* hizo zipo, Mhe. Abubakary tumesoma darasa moja, tumesomesha na mwalimu mmoja na anayajua hayo.

Pili suala langu ni kuwa, tukifungua Katiba ya Zanzibar ukurasa wa 11kifungu Nam. 19.(1) kwa ruhusa yako naomba kunukuu kinasema kuwa:

> "Kila mtu anastahiki kuwa na uhuru wa mawazo wa imani na wa uchaguzi katika mambo ya dini pamoja na uhuru wa kubadilisha dini na imani yake"

Waislamu tunajua kuwa hakuna dini isipokuwa ni dini ya Kiislamu tu, hiyo tunajua. Lakini katiba imeandika hivi kama kuwa aliyeandika sio Muislamu. Hakuna asiyejua kuwa wakati wa mchana watu kupita wakila ovyo ni kitendo cha kuvuruga Ramadhani yetu.

Kwa hivyo Mheshimiwa kwa sababu yeye ni Mhe. Waziri wa Katiba, na hivi sasa keshaunda Tume kwa kuweka mambo sawa, yakenda kinyume na kifungu hichi cha Katiba. Kwa nini hatumii rai ya kuondoa hichi kifungu kwanza kuwa dini iheshimiwe halafu tena ndio Tume yake ifanye kazi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakubaliana sana na Mhe. Salum kwamba tulisoma pamoja, darasa moja, mwalimu mmoja, Bonderemko. Lakini katika kusoma kuna *capacity* ya ku- *grasp* yale uliyosomeshwa. Sasa nafikiri tulivyosomeshwa hakufahamu vizuri, ninavyofahamu mimi hapo tuliposomeshwa, tuliambiwa kwamba katika *hormones* hizi kuna *stimulate* ambazo zinafanya hizo *hormones* kuongezeka. Sasa nafikiri *stimulate* zake yeye na Mhe. Saleh zina matatizo. Nahiyo sibishi kwa sababu..

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ni ile ile ibara ya 58 kifungu kidogo cha (1) cha kanuni yetu, kuwa na uhakika na unalolisema. Mheshimiwa nimelisema neno hili kwa uhakika, kwa sababu mwanamme yeyote aliye mzima wa afya anapomuangalia mwanamke ambaye hakuvaa vizuri yaani *optic nerves* yaani *nerves* zilizokuwepo kwenye macho zinachukua hisia kupeleka katika *central nerver system, katika. hypothalamus of the brain than hypothalamus of the brain* inatoa *testosterone hormones* anakenda zake katika *testis* kufanya *eraction* ya *reproductive organ* ukishafika hapo saumu hapana. Ukiwa mwanamme yeyote ni mzima, labda awe ni mbovu lakini mwanamme yeyote aliyemzima ataona.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa kuendelea na suala hili. Mhe. Spika, jawabu langu ni lile lile kwamba hizi *senses* hizi inategemea watu wengine *senses* zao zina matatizo, na hao ndio hawa tunaopigana nao vita kwa kubaka, mara utasikia wamebaka, sio sote tunaobaka. Mhe. Spika, sio sote tunaobaka ni baadhi ambao wana matatizo ya *nerver* kama hawa.

Jengine Mhe. Spika, alilozungumza Mhe. Salum nakubaliana na kifungu alichokitaja lakini hapa kama alinifahamu vizuri nilisema hii Kamati itakaa na kujadili kutizama mawazo yote hayo tuliyopewa. Na tunapopeleka mapendekezo yetu serikalini ni pamoja na kuangalia hivi vifungu vya katiba je, vinakiukwa au havikiukwi. Sasa hapa ndio tutaishauri serikali nini tufanye ili suala hili liende kwa vizuri.

Mheshimiwa nakushukuru.

Nam. 18

Tatizo la Ukosefu wa Maji Vijijini:

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Hufuma ya maji nchini imekuwa na changamoto nyingi ikiwemo baadhi ya maeneo kukosa kabisa huduma hiyo hasa vijijini. Je, Wizara imechukua hatua gani kuliondoa tatizo hilo hasa vijijini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yaoko naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 18 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa huduma ya maji ina changamoto nyingi hali ambayo serikali kupitia Wizara yangu imechukua juhudi kwa kiasi kikubwa kuwapatia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama. Kwa sasa huduma ya maji vijijini imeimarika kiasi, maeneo machache yaliyobakia serikali kupitia ZAWA bado inaendelea na mpango ya kuwaondolea tatizo la upatikanaji huduma ya maji safi na salama pamoja na nguvu za Wizara Ardhi, Makaazi, maji na nishati. Aidha baadhi ya vijiji vinategemea kunufaika na huduma ya maji kutoka mradi wa benki ya Afrika ya (ADB) ambao kwa hivi sasa umo katika hatua za Zabuni.

Mhe. Spika, miradi mengine ni mradi wa ACRA, mradi wa Kizimkazi, mradi wa TASAF, mradi wa Chukwani, mradi wa Maziwa Ng'ombe, mradi wa Kojani, mradi wa Nungwi. Mhe. Spika, ikimalizika miradi hii tunategemea huduma ya maji safi na salama itapatikana katika vijiji.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa jibu nililopata kutoka kwa Mhe. Naibu Waziri. Lakini katika bajeti iliyopita tulipopitisha Wizara hii katika kitabu chake ukurasa wa 88 kuna jaduweli aliitoa ambayo inaonesha vijiji vitakavyofaidika na mradi wa usambazaji wa maji vijijini kwa Pemba na Unguja. Unguja kuna vijiji 15 na Pemba ni 10 kikiwamo Kisiwani na Mtambwe Kaskazini, hivyo vilikuwa katika jimbo la Mtambwe. Lakini tokea wakati huo mpaka hii leo hatujaona ishara yoyote.

(a) Je, maelezo yale ya bajeti yalikuwa bado hayajakuwa katika utaratibu wa kuwa yalikwisha kupangiwa kuwa yatakuwa, haya yalikuwa ni maneno tu.

(b) Bado kuna vijiji vingi sana sio vichache kama anavyosema Mhe. Naibu Waziri ambavyo havikuingizwa katika kitabu hiki na havina huduma ya maji na watu wanahangaika sana. Vijiji hivi Mhe. Waziri anatupa ushauri gani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumsaidia Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa katika suala mama lililoulizwa.

Mhe. Mwakilishi aliyeuliza suali alizungumzia kijiji cha Mtambwe na vijiji vyengine kadhaa kama vilivyotiwa katika kitabu cha bajeti. Nakubaliana naye kwamba vijiji hivyo bado havijapata maji na tatizo la maji kama alivyosema yeye mwenyewe muulizaji linachangamoto nyingi. Na wala si rahisi changamoto hizi kuzimaliza kwa kipindi cha mwaka mmoja wa bajeti.
Vijiji ambavyo havikuguswa katika mwaka huu wa bajeti vitaingizwa tena katika bajeti ya mwaka ujao. Lakini hali kadhalika kwa mfano kijiji cha

Mtambwe hakukieleza vizuri Mtambwe ipi lakini nina hakika na ninajua katika miradi ya Msaada kutoka Uchina ya Pemba na Unguja, Kijijij cha Mtambwe kimo katika miradi hiyo.

Kwa hiyo kama jibu lilivyozungumza kuna miradi mingi sana ya maji ya ACRA ya UDB hakutaja Wachina, hakutaja Wajapani, lakini kuna miradi mingi sana ya maji iko njiani inakuja na imefika katika hatua nzuri sana sasa za kutafuta wakandarasi wa kuanza kazi ya kuchimba visima, kutia pampu na kusambaza mabomba katika maeneo ambayo bado hayajapata maji.

Nataka nikiri kwa mwaka huu si kweli kwamba tatizo la maji la nchi hii linaweza kumalizika moja kwa moja. Suala lilikuwa serikali inachukua juhudi gani. Serikali inachukua juhudi kubwa sana katika maeneo yote, tunaendelea kuchimba visima na kupata misaada mbali mbali. Tuhakika kwa mwaka huu hatutomaliza matatizo yote, lakini asilimia kubwa sana ya matatizo yatakamilika kutatuliwa kama tulivyoanza kuyaona hivi sasa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi hii ya asubuhi kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza.

Atakumbuka Mhe. Naibu Waziri bajeti iliyopita kulitengwa fedha kwa makusudi ili kuondoa tatizo hili la maji ambazo kama shilingi milioni 600, kama nimekosea atanisawazisha. Lakini je, mpaka hivi leo nauliza hizi fedha zimeshaanza kutumika na kama hazijatumika ni kwa sababu gani ambazo mpaka leo zipo katika *account* tu zimekaa wakati huku wananchi wanapata matatizo ya maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, narejea kusema kwamba kweli pesa zimetengwa katika bajeti, kati ya hizo zipo ambazo zilizoanza kutumika, miradi tunaiyona. Kwa mfano mradi wa ACRA kulikuwa kuna *contribution* ya serikali. Pesa hizo ndizo zilizotumika katika kutekeleza ile *contribution* ya serikali. Na mda wa fedha haujamalizika, tama ya kuzitumia na nyengine ipo.

Mhe. Spika, nataka nilirejee nililolieleza, si rahisi nataka nikiri kabisa kwamba si rahisi kwa matatizo au changamoto za maji Unguja na Pemba zilizopo, haziwezi kumalizika kwa mwaka mmoja. Hizi zilikuwepo, tumezikuta, zipo na tutajaribu kuziondosha kadiri tutakavyoweza. La msingi akubali Mheshimiwa Naibu Waziri aliyoizungumza ambayo mengine anatafutwa mkandarasi, mengine inamalizika kuchakachuliwa kwa maana ya kuzingatiwa na mengine karibu mwezi wa Machi itaanza.

Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa avute subira ili atupe nafasi kuiyona hii miradi tuliyoizungumza. Na mengine namuahidi tutaifungua katika siku inayoitwa "Siku ya Maji Duniani". Mengine katika hii itafunguliwa kama mradi wa Kizimkazi, mradi wa Maziwa ya Ng'ombe tumefungua juzi, mradi wa Konde utaanza karibuni. Miradi ni mingi, changamoto ni nyingi, jitihada ni kubwa tunazozichukua katika kulipunguza tatizo la maji, hatuwezi kulimaliza. Kwa hivyo namshukuru Mhe. Mwakilishi kwa suala lake nalichukulia kwamba ni kumbusho, lakini na yeye namuomba anipe stahamala ya mda, pole pole mradi baada ya mradi tutautekeleza.

Nam. 28

Ujenzi wa Barabara za Lami ya Kuteleza

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Hali ya ujenzi wa barabara zenye lami ya kuteleza inahatarisha mno usalama wa vyombo vinavyotumia barabara hizo. Mfano barabara kutoka Kilimani (Hospitali ya Al-Rahma) hadi Gofu.

Mhe. Waziri, jitihada gani zitachukuliwa ili kuepukana na ujenzi wa aina hiyo ili kuepuka ajali.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 28 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Wizara yangu haijapokea taarifa yoyote ya ajali iliyosababishwa na ujenzi wa barabara hivyo au kwa sababu zilizoelezwa katika suala hili. Ni mategemeo yetu kwamba wadau wetu hasa bodi ya usala barabarani utalipokea kwa kutathmini suala hilo ili kutufikishia kwa hatua zaidi.

Mhe. Spika, Wizara yangu haitokuwa na uwezo wa kuchukua hatua zozote kuhusiana na suala hilo kwani bado hadi muda huu halijajitokeza. Aidha, Wizara yangu inaahidi kupokea kila aina ya ushauri na ushirikiano katika kuimarisha miundombinu ya nchi yetu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumuuliza suali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa barabara hiyo kutoka Kilimani hadi Bopwe inateleza kutokana na utandu wa kijani uliopo. Je, Mhe. Naibu Waziri ni sababu gani hasa inayosababisha kufanya utandu huo wa kijani barabara ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, barabara hii kipande hicho anachokisema haitelezi, lakini napenda nikiri kwamba upande wa mkono kushoto kama unayeelekea mjini kutoka eneo la msikiti wa Kilimani kuna matumizi mabovu ya wananchi wetu wanaotumia huduma za maji yanayotiririka katika barabara. Maji hayo yanayotiririka kwenye barabara nyingi yanakuwa ni maji machafu ndio yanayopelekea kuonekana kama kuna utandu kutokana na maji hayo. Lakini sio kama rangi hiyo inasababishwa na ujenzi mbovu au lami iliyotumika kama ni mbovu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alikiri katika jibu lake mama kwamba hajapata taarifa ya ajali yoyote katika eneo lile lakini jana ziligongana gari tatu kwa pamoja. Je, taarifa hii hana na wamefanya uchunguzi ni nini hasa kilichojitokeza ni uzembe wa madereva, kuteleza kwa barabara au ni kitu gani kilichotokea.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika jibu mama tumeeleza kwamba hatujapata taarifa ya ajili iliyosababishwa na gari kuteleza kwa ujenzi wa barabara kipande kile, naendelea tena kurejea majibu yangu hayo kwamba ajali hizo sisi kama Wizara ya Miundombinu tutashirikiana na Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi na kuthibitisha kwamba ajali hiyo ya jana imesababishwa na gari kuteleza ama ni makosa ya kiudereva.

Nam. 5

Fidia kwa Wanaoanguka Mikarafuu

Mhe. Raya Suleiman Hamad - Aliuliza:-

Mhe. Waziri, Serikali ina mpango gani wa kurudisha utaratibu wa kuwalipa fidia watu wanaopata ajali ya kuanguka mkarafuu wakati wa kuvuna zao hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa sasa Shirika halina uwezo wa kuwalipa fidia waathirika wanaoanguka na uchumaji wa karafuu kutokana na asilimia ndogo ya fedha wanayoipata kutokana na ununuzi wa bidhaa hiyo. Lakini Wizara ya Afya inayo mpango mzuri wa kuwashughulikia wale wote wanaoanguka na mikarafuu hadi kuwapeleka Tanzania Bara kulingana na athari wanayoipata anapoanguka ili kupata matibabu yanayofaa. Aidha, serikali kupitia kupitia

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaandaa warka wa kuanzisha mfuko wa kuendeleza karafuu ambao pamoja na mambo mengine mfuko huo utakuwa na jukumu la kuwahudumia wale wote wanaopata ajali za aina hiyo.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, naombab kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba kuokoa zao la karafuu ni kuokoa pato la kitaifa, na mpango huu wa kulipwa watu wanaoanguka mikarafuu ulikuwepo siku nyingi sana, na leo ukianguka mkarafuu ikiwa mtu mzima au mtoto tayari unasababisha ulemavu. Je, ni sababu zipi wizara isirudishe taratibu hizo ya kuweza kuwalipa mafao watu hao wanaonguka.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nimesema katika jibu langu kwamba kutokana na asilimia ndogo tunayopata kupitia Shirika hili la ZSTC ndio maana huduma hizi hazifanyiki kwa shirika hilo. Lakini Wizara ya Afya inawahudumia wanaoanguka kwenye miti ya mikarafuu, lakini pamoja na hayo Mhe. Spika, bado kuna utaratibu mzima wa kuanzisha mfuko huu wa kuendeleza zao la karafuu katika mfuko huu ndio tunategemea kwamba kutawekwa utaratibu maalum wa kuwahudumia hawa ambao watakuwa wanaanguka kutoka kwenye mikarafuu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwamba fedha walizotoa kununulia karafuu ni fedha nyingi na bei nzuri, lakini napenda nimuulize swali baada ya kumpa taarifa kwamba wengi waliofaidika na fedha hizi ni wale wenye ile mikarafuu, lakini wanaoanguka ni wachumaji. Je, wizara haioni kwamba kwenye hiyo asilimia 20 katika mpango wake kuweka asilimia maalum kwa ajili ya kuwahudumia hawa ambao wengi wao hiyo mikarafuu hawana au sio wanaozipata hizo fedha baada ya karafuu kuuzwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, pamoja na sababu nyengine ni hii aliyoisema yeye Mhe. Mwakilishi ya kwamba fedha wanazopata ZSTC ni ndogo, lakini wanaoanguka mikarafuu wengi ni wale vibarua.

Mhe. Spika, wizara imeliopa hilo ndio maana ikaona ipo haja ya kuanzisha mfuko huu wa kuendeleza zao la karafuu, ili miongoni mwa mambo mengine pia kuangalia haja ya kuwahudumia hawa wanaoanguka kutokana kwenye mikarafuu.

Nam. 25

Mashine ya Kusukuma Maji kwa ajili ya Ukulima wa Mboga mboga

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Inasemekana kuwa mashine ya kusukumia maji kwa ajili ya ukulima wa mboga mboga ambayo ilikuwa inapelekwa Kangani Pemba ilizama katika ajali ya MV. Spice Islanders.

a) Je, jambo hilo ni kweli.

b) Kama ni kweli, na kwa vile wananchi waliweka matumaini, serikali ina mpango gani wa kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, ni kweli *pump* ya umwagiliaji maji iliyokusudiwa kwenda Pemba kufanya kazi katika bonde la Machigini Wilaya ya Mkoani ilikuwemo katika MV. Spice Islanders na ilizama pamoja nayo.

b) Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kwamba serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF II) imekubali kutoa pesa kununu mashine mbadala ya kusukumia maji kwa ajili ya ukulima wa mboga mboga kwa lengo la kuwawezesha wakulima kuongeza mavuno na tija hatimae kupunguza umasikini.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wakati huu ni wajua kali na kwa kuwa wananchi sasa hivi wamekaa tu hawana zile kazi za kujishughulisha, na kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kweli kwamba mashine hiyo ilizama na MV. Spice Islanders. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba hii ni kuwarudisha nyuma wananchi hawa katika kilimo chao hicho.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, ajali ni ajali serikali haijakusudia itokee ile ajali, tuishukuru sana serikali kwamba ikubali kutoa fedha nyengine kununua *pump*

hiyo. Najua kwamba sasa hivi ni wakati wa kiangazi na watu hawana cha kufanya lakini wastahamili kidogo maana sasa hivi lazima itafutwe mashine mpya kwa kazi hiyo na sio kuwarudisha nyuma wananchi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Spika, lengo na dhamira *GNU* ni kupunguza umasikini pamoja na kuongeza kipato kwa wananchi wake, na kwa kuwa wananchi wa Kangani wameekeza katika kilimo naamini kwamba wako mbioni wanatekeleza agizo la *GNU*. Je, Mhe. Waziri nadhani ingekuwa vyema hatua za dharura zikachukuliwa kwa kupelekewa hawa akina mama mashine hiyo kusudi wakaweza kutekeleza dhamira ya Serikali yetu hii ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, ni kwamba subra inahitajika kidogo kwa sababu mfuko wa TASAF ushaanza kufanya kazi hivi sasa. Kwa hivyo, huko ndio kuharakisha kwenyewe.

Nam. 75

Zanzibar Kujiungana *FIFA*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Kwa sasa Zanzibar ni Mwanachama wa *CECAFA* na *CAF*. Je, kuna uwezekano wa Zanzibar kujiunga na *FIFA*.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 75 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Zanzibar ni mwanachama wa *CECAFA* na pia ni Mwanachama wa *CAF*, suala la Zanzibar kujiunga na *FIFA* bado hatujakata tamaa kwani zipo nchi nyingi zilijaribu kutuma maombi tena hata zaidi ya mara 2 au 3 hatimae zilifanikiwa. Jitihada zaidi zitafanyika kati ya wizara yangu kwa kushirikiana na *ZFA* na *TFF*, pamoja na wadau wengine. Tunaomba Wajumbe wa Baraza hili nao watuunge mkono katika suala hili hasa utakapofikia wakati wa kufanya marekebisho ya Katiba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kama ipo haja ya kushirikiana na waziri aliyekuwa wa michezo mwaka 2003-2004 akakupa mbinu au njia alizotumia hata tukaupata uanachama wa *CAF*.

b) Mhe. Naibu Waziri pia huoni ipo haja hivi sasa Zanzibar kuwa na wanachama wake au wajumbe katika Kamati ya *TFF*.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kwamba kipindi cha bajeti iliyopita swali hili tulililitolea ufafanuzi wa kutosha kwa sababu Mhe. Mwakilishi ulikuwa hupo lakini kwa faida ya wananchi nasema kwamba Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Rais wa *FIFA* walikaa pamoja kuzungumza suala hili la *FIFA*, lakini hawakulipatia ufumbuzi. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Mwakilishi kwa kushirikiana na wananchi wote uwe ni mpigaji depe mkubwa wakati wa kubadilisha Katiba suala hili ulipe kipaumbele.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi wa Kisiasa ya 2011

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kupata fursa hii kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu. Kwanza naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza walioshiriki katika mjadala huu. Mhe. Spika, kwa kweli lazima nikiri ulikuwa na hoja nzito, nyingi na kama serikali hatuna budi kukaa chini kuzizingatia, kuzitafakari na hatimae kuzitolea majibu ipasavyo.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna maoni, kulikuwa na waheshimiwa wengine walitoa maelekezo, kulikuwa na waheshimiwa wengine walikuwa wana maswali ambayo tunahisi kama hawajafahamu kutokana na mswada wenyewe. Mimi nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wamechukua jukumu la kunisaidia kujibu hoja na kutoa ufafanuzi mwingi pale ulipo.

Mhe. Spika, kwa mantiki hiyo kwamba hoja zilizotolewa ni nyingi na ni nzito na kama serikali inabidi tukae tuzifanyie kazi na kuzijibu ipasavyo, basi kama ilivyo katika Kanuni ya Baraza la Wawakilishi kifungu cha 84 (1) na utaratibu wa kuzungumzia miswada katika Baraza Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba nitajibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe baada ya kupita angalau muda wa saa sita.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kanuni hiyo hiyo ya 84 (1) naomba niisome. "Endapo mswada umesomwa kwa mara ya kwanza na majadiliano kuhusu ubora wa misingi ya mswada huo yamekwisha, waziri au mjumbe mwengine aliyehusika na mswada huo atatoa taarifa kwamba atajibu hoja za wajumbe mara tu baada ya michango ya wajumbe au baada ya kupita muda usiopungua masaa sita".

Mhe. Spika, sasa mjadala huu michango ya wajumbe ilimalizika jana kwa hivyo saa sita zitakuwa zimeshapita na amepata usiku mzima wa kujiandaa leo asubuhi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama tunataka kufasiri sawa sawa kanuni hii basi ilivyo waziri ameshapata muda wa zaidi ya masaa sita ili kujibu hoja zetu na baadae Baraza hili lipate kufanya kazi yake ya kuamua kuhusu mswada huu. Mhe. Spika, naomba tuzingatie kanuni zetu.

Mhe. Spika: Ni kweli jana tulimaliza mjadala kunako saa 1:45 barabara na kwa kutegemea kwamba leo asubuhi baada ya kipindi cha maswali basi Mhe. Waziri angeweza kutoa majumuisho ya mswada huu, kutoka jana hadi leo ni kweli masaa sita yametimia lakini jana ilikuwa usiku na ukweli wa mambo ni jambo ambalo linahitaji majadiliano ya serikali karibu yote. Hilo la kwanza.

Jambo la pili ni kwamba pamoja na watendaji haikuwa rahisi kutokea jana pale usiku kuweza kuifanya kazi hiyo, na ndio maana leo hii kwa sababu kama ingelikuwa jana tulimaliza mapema lakini ule muda wa kusema angalau kwamba sasa waziri hebu njoo utoe ombi haukuwepo, ilikuwa barabara saa 1:45. Kwa hivyo, baada ya pale na kwa kuwa kazi ilikuwa sio ndogo sikuona haja ya hata kumuomba waziri labda atoe maelezo kwa sababu muda wenyewe ulikuwa umekwisha kabisa. Waheshimiwa Wajumbe kama tungefanya hivyo ingelibidi sasa tuombe ridhaa yenu kuzidisha muda kwa ajili ya kupata maelezo kwa sababu muda wenyewe wa kawaida ulikwisha.

Waheshimiwa Wajumbe mimi naona kwamba kwa madhumuni ya kufanya jambo hili liwe zuri kama mpaka ile jana hana majibu kwa sababu tuliondoka hapo usiku sote tumeshuhudia hilo. Mimi nadhani isiwe tatizo tukubali mimi alinipa taarifa hiyo na kwa kweli mimi nakubali hiyo taarifa jambo hili tuliahirishe ili apate muda wa kuweza kutoa majibu kwa sababu ninavyoelewa na ndio utamaduni katika Baraza letu hili, tofauti kidogo na Bunge. Maana Bunge kuna muda maalum ambao mawaziri hawa huwa wanapewa kujibu hoja, wakati mwengine pengine nusu saa, mliokuwa Bungeni mna maarifa zaidi. Lakini kwetu tuna kawaida yakujibu mjumbe baada ya mjumbe au kuwakusanya wajumbe wenye hoja ya aina moja ukawajibu kwa pamoja halafu ndio utamaduni ambao tumekuwa tunaufuata.

Waheshimiwa Wajumbe nathubutu kusema katika Baraza letu tuna demokrasia pana zaidi kuliko ilivyo katika vyombo vyengine kwa sababu ya kumridhisha kila mjumbe na hoja ile ambayo ameitoa. Na kwa sababu utamaduni huo sio mbaya ni mzuri kwa ajili ya kuweka masuala yetu vizuri, mimi nakubali kwamba tumpe muda ili aje atoe majumuisho mazuri ya kutosha na pale ambapo kufuatana na yale yaliyotokea humu ndani kutokana na wajumbe mbali mbali upande wa *backbencher* na serikali yanayohitaji kurekebishwa yawekwe vizuri ili tufikie pahala tuwe na kitu ambacho kinakubalika. Hii taarifa alikuwa ananipa mimi kimsingi nakubali hiyo taarifa tumpe muda ili afanya hiyo kazi. Kwa hivyo, nakubali kwamba jambo hili na kwa kuwa hivi sasa tayari ni saa tano karibu shughuli hii ifanyike siku ya Jumatatu.

Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu shughuli hii inaakhirika kiasi hicho na muda upo wa kuweza kuendelea na kazi iliyopo ndani ya *order paper* nafikiri Katibu tuendelee.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba mawaziri wasiwe na wasi wasi kwa sababu nakiheshimu kiti chako. Mhe. Spika, jana ulituahidi baada ya hoja ambayo niliizungumza juzi kuhusiana na suala la ombi la Jamhuri ya Muungano la kutaka kuongezewa eneo la mipaka ya bahari kuu kwa ajili ya matumizi yake ambayo linakwenda kinyume na maamuzi ya Baraza lako la Wawakilishi la mwaka 2009 tukataka maelezo ya serikali. Mhe. Spika, ulituahidi kwamba ilikuwa maelezo hayo yatoke jana lakini kwa sababu waziri muhusika alikuwa katika dharura ya kushiriki mazishi suala hilo lingefanyika leo. Kwa hivyo, katika *order paper* hatukuliona tukadhani labda kwa utaratibu mwengine wakuletewa lakini bado tunaona hakuna maelezo yoyote, Mhe. Spika, naomba muongozo wako.

Mhe. Spika Waheshimiwa Wajumbe ni kweli suala hili tuliliahirisha kwa sababu waziri muhusika alikuwa amepata msiba na nilipoingia asubuhi nilikuwa namtafuta kabla ya kuingia kwenye ukumbi ili kuhakikisha kama yupo tayari, bahati mbaya nadhani alichelewa kidogo nimeingia ukumbini kabla ya kuonana nae. Kwa hivyo, basi tupate taarifa kama jambo hilo anaweza kuwa tayari hivi sasa baada ya shughuli ya msiba ile au kama vyenginevyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maelezo machache kuhusu suala la maombi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yakuongezewa eneo la mipaka ya EEZ kuendea upande wa Magharibi kwa *two hundred miles*. Nasema kidogo pana mchanganyiko wa hoja hapa ambapo nitatoa taarifa hii *with assumptions* kwa sababu hili suala ni la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Mimi si waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wala katika Baraza hili sikupewa mamlaka ya kuisemea Zanzibar kwa mambo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hilo la mwanzo ningependa niliweke wazi kabisa kwa sababu nitakayoyaeleza pengine yatazua hoja sitaweza kuijibia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama suala linatakiwa nieleze kile ninachokijua nitaeleza.

Mhe. Spika, nilipata taarifa kwamba suala hili linapelekwa *UN* kwa mazingatio kwamba Tanzania sasa hivi imefika wakati inastahiki kuongezewa eneo lake la Bahari Kuu sasa liwe zaidi ya zile meli za baharini 200 zilivyo sasa, na badala yake ziongezwe *mail* 200 zaidi ili ziwe *mail* 400.

Nilipata taarifa kwamba nilitakiwa nishirikiane na waziri wa Tanzania kwenda katika mkutano huo wa New York ili kwa pamoja tukawasilishe ombi hili la kuongezewa eneo la mipaka. Kwa sababu ya vikao vya Baraza niliomba badala yangu nimpeleke msaidizi wangu ili mimi niendelee kuhudhuria vikao vya Baraza. Hilo nikakubaliwa na nikampeleka mmoja katika wasaidizi wangu wakubwa kushirikiana na yule ambaye anakwenda kutoa mada kule. Kwa hivyo, kwa kiasi fulani nalijua nimeshirikishwa, tumeshirikishwa.

Kinachokwenda kuzungumzwa ambacho hakihitaji maamuzi ya hivi sasa ni kuwasilisha ombi na sio kuwasilisha na kujadili ombi ni kuwasilisha ombi. Ombi likishawasilishwa Tanzania itapangiwa siku au mwezi kwenda kushiriki katika kulijadili na hatimaye likubaliwe au likataliwe.

Mhe. Spika, kwa taarifa ya magazeti hayo hayo ambayo wenzangu wameyasoma mjadala huo au ombi hilo litajadiliwa mwezi wa Julai, kama taarifa hizo ni sahihi basi zichukuliwe kwamba ni sahihi, kama sio sahihi sio taarifa zangu mimi, mimi nimesoma kwenye gazeti.

Waraka umeandikwa nimeletewa nakala ya waraka huo nimeusoma, nimeufahamu, waraka unazingatia ombi kwa sababu ombi hili inaonekana lilikuwepo zamani Tanzania imeomba zamani suala hili sasa hivi Tanzania imearifiwa kwamba ule wakati wa kuwasilisha ombi lenu sasa hivi umefika, kwa hivyo, mje muwasilishe. Ukatoka ujumbe kwanza ikachaguliwa timu ya kuandika ikaandika watu wangu wameshirikishwa katika maandiko hayo sasa ikachaguliwa timu ya kwenda kulipeleka hilo ombi. Kama nilivyosema mimi nikadharurika nikampeleka msaidizi wangu tena *senior* yuko huko hivi sasa.

Kwa kiwango kikubwa nilivyofahamu ombi litawasilishwa na limeshawasilishwa litajadiliwa mwezi wa Julai, hapo tena ndio mjadala wa kukubaliwa au kutokukubaliwa utatoa maamuzi. Ukikubaliwa suala hili

litarejeshwa Tanzania kwa kuridhiwa pamoja na zile nchi ambazo zinapakana na zile *mail* 200 zilizoko sasa hivi. Kwa mfano, Seychelles, Mauritius, Madagascar, Re Union na kadhalika. Kwa pamoja sasa nchi hizi pamoja na Tanzania zikiridhia sasa hiyo hoja itakuwa *authentic* na imekubaliwa.

Kwa hivyo, hoja ni kwamba tumekwenda kuwasilisha hatukwenda kujadili, tumekwenda kuwasilisha siku ya kujadiliwa imeshapangwa, mwezi wa kujadiliwa umeshapangwa, itabidi timu iende tena sasa kwenda kushiriki katika mjadala na zile nchi zote zilizopakana na *EEZ* zitashiriki na hizo ndizo zitakazopelekea maamuzi sahihi ya baadae.

Mhe. Spika, kumezungumzwa maazimio, kulitoka maazimio kwa bahati mbaya mimi sinayo. Mhe. Ali Mzee aliyeteuliwa na rais mwenye Jimbo la Ikulu alipokuwa anachangia hoja hii aliomba basi hayo maazimio yangegawiwa wajumbe wakayapata. Mimi nimekuja sikuliona nimeuliza jibu hakuna kilichogawiwa, kama kipo kilichogawiwa ningeomba na mimi nipatiwe.

Sasa mimi sikuifahamu hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu nilikuwa niko nje, nilipoingia ndio nikamkuta anamalizia akitaka maelezo ya serikali kuhusu suala hili kama Serikali ya Zanzibar inajua. Kama hivyo ndivyo na kwa kiasi cha tafsiri kwamba waziri ni serikali naweza nikasema Serikali ya Zanzibar inajua. Lakini kwa tafsiri kwamba serikali maana yake ni *cabinet* basi *cabinet* haijui kwa hivyo, Serikali ya Zanzibar haijui. Suala hili halikupelekwa katika *cabinet* na halijajadiliwa, hili suala pengine lina umri wa miezi miwili au mitatu tokea lije.

Nataka nimalizie kwa kusema tena kwamba, kilichowasilishwa *UN* nakijua, kama waziri maana yake ni serikali nakijua na kwa hivyo serikali inajua, nakijua kwa maana tunakwenda kuomba nyongeza ya *mail* za baharini 200 zaidi ya zile tulizonazo 200 kwa upande wa Magharibi. Hili suala halijagusa Zanzibar na sikuona mahala popote kwamba pamezungumza *including* Zanzibar katika maandishi, inawezekana imeandikwa katika magazeti, maandishi ninayo.

Mhe. Spika, nitakuomba uniruhusu Jumatatu nikukabidhi andiko rasmi lililopelekwa *UN* ili na wewe upate nafasi ya kuliangalia na kwa mujibu wa protokoli kwa kuwa mimi ni waziri itabidi pia nimkabidhi kwanza Makamo wa Pili wa Rais nikisha nikukabidhi na wewe uliangalie. Kilichopelekwa ni ombi la kuongezewa eneo la *mail* 200 Magharibi ya *EEZ*. *EEZ* Mhe. Spika, inaanza mail za baharini 200 kwa Zanzibar kutoka ufukweni haianzi kwenye ufukwe inaanza *mail* 200.

Kwa kiasi nilivyoelewa suala la *EEZ* ni suala la Muungano si suala la Zanzibar peke yake wala si suala la Tanzania Bara peke yake ni suala la Muungano. Kwa maana hiyo, taarifa niliyonayo niliyotakiwa niwasilishe kwa mazingira ambayo kidogo yamenibabaisha siyaelewi ndio hiyo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba radhi sana kwa sababu mara nyingi ukishanyanyuka kwa heshima ninayokupa huwa sipendi niingilie kati, lakini kwa suala hili na namna lilivyojibiwa naomba kidogo.

Mhe. Spika, sijui niichukulieje kauli ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati kama ni kauli ya waziri au vipi, lakini niseme kwamba, kwa mujibu wa kanuni ya 43 Kauli za Mawaziri huwa hazijadiliwi, lakini kwa uzito wa suala hili na majibu haya nia yetu ikiwa njema ya kuisaidia serikali mimi nilikuwa naomba nitumie kanuni ya 151 kutenga kando kanuni ili Mhe. Spika, uturuhusu kwa muda mfupi tu, tulijadili suala hata kika cha asubuhi.

Kanuni ya 151 inasema kwamba:

> "Kwa idhini ya Baraza yoyote kati ya kanuni hizi inaweza kutengwa kando kwa madhumuni mahsusi baada ya mjumbe yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo".
>
> "Hoja inayotolewa kwa kanuni hii haitatolewa taarifa na itaamuliwa bila ya mabadiliko wala majadiliano yoyote".

Sasa Mhe. Spika, naomba tutenge kando kanuni ya 43 inayohusu Kauli za Mawaziri kutojadiliwa ili hili tulijadili japo kwa muda mfupi kabisa kusudi Baraza lako litoe maelezo mahsusi kwa serikali nia yetu ikiwa ni njema baadae serikali ije itujibu kwa marefu na mapana hapa kuhakikisha kwamba tunalinda maslahi ya Zanzibar na watu wake na tunalinda maamuzi ya Baraza lako tukufu ya mwaka 2009 nikikuhakikishia suala hili si jepesi huko nje limeshajadiliwa sana, tunahojiwa sana. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, kama kanuni inavyosema hakuna mjadala au tuhoji kwa kukubali kuweka kando kanuni hii ili kujadili suala hili. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kabla ya kutoa nafasi ya kuuliza maswali kuna jambo moja nadhani inaelekea pengine taarifa ya kile ambacho tumekiamua humu ndani kama alivyoeleza mwenyewe Mhe. Waziri haikumfika sawasawa.

Kuna jambo ambalo nataka nikiri kwamba ofisi yangu itakuwa haikutekeleza na jinsi vile ambavyo taarifa haikumfika sawa sawa hata hilo azimio lenyewe pengine Mhe. Waziri hakufahamu ni lipi.

Azimio lililotajwa kwamba lingetayarishwa na wakapewa Waheshimiwa Wajumbe ni lile azimio tulilopitisha mwaka 2009 kuhusiana na masuala ya utafiti wa mambo ya mafuta, ikawa kuna maeneo yale yaliyoingia katika hili eneo la *mail* 200 ambalo ni eneo la Muungano. Katika maazimio yale nakumbuka kwamba tulikubaliana katika hilo azimio kuwa jambo hili nalo waombwe wenzetu libakie kushughulikiwa na upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sasa hilo ndilo azimio lenyewe ambalo linahusu Wizara ya Ardhi, Makazi, Maji na Nishati, wakati ule ilikuwa ni Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Kwa hivyo, kwa ajili ya kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe je, ombi hili lililofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kule UN kuongezewa eneo hili. Mwenzetu mjumbe alipata hofu je, haitaathiri yale maamuzi ya azimio tulilotoa? Tukasema kwamba suala hili linahusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni vyema serikali yetu ikakae ione vipi jambo hili kama linaathiri au halitoathiri suala la maazimio yetu ambayo tulijiwekea.

Bahati mbaya Mhe. Waziri hakuwepo lakini tukaelekeza kwamba jambo hili ingefaa serikali ituletee taarifa, taarifa anayoleta Mhe. Waziri ni kwamba wizara yao imeshirikishwa lakini mjadala katika *cabinet* kwa maana ya Baraza la Mapinduzi inaonekana haukuwahi kufanyika na kumbe hili ombi lipo kwa muda mrefu huhko nyuma. Hii ilikuwa ni sasa wameambiwa tu kwamba muda wenu sasa wa kuja kuwasilisha kama nimefahamu sawa sawa ndio kipindi hiki ambacho kwa ushirikishwaji waliopewa na wizara ile inayohusika ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio waziri akatuma mjumbe badala ya kushiriki yeye mwenyewe.

Sasa nadhani maazimio haya bila shaka itakuwa yapo kwenye wizara ya Mhe. Waziri, lakini maazimio haya pia yapo hapa katika ofisi yetu ya Baraza la Wawakilishi. Mimi kwa madhumuni ya wajumbe wetu hapa nikasema watendaji wetu hapa watoe yale maazimio ili kila mmoja Mhe. Mjumbe jambo hili litapokuja kutolewa taarifa yale maazimio anayo ambayo itamuwezesha mjumbe kuuliza maswali kufuatana na yale maazimio yalivyo.

Kwa kuwa jambo hili halikuwahi kujadiliwa kama alivyosema katika *cabinet*, mimi nadhani bado tutoe muda kwa serikali ili suala hili walitizame kama kuna haja ya kuitana kwenye *cabinet*, lakini katika mkutano huu watupatie taarifa nyengine chini ya kauli ya mawaziri ambayo sasa tutapata hii nafasi ya kuja kuuliza maswali. Nielekeze pia wale watendaji wangu lile azimio walitoe ili

Waheshimiwa Wajumbe wote wapate na pale muda utapofika kuja kutoa kauli hiyo katika mkutano huu basi watatwambia sasa nini serikali ambacho wamejipanga kama kulichukua kwenye *cabinet* au maana yoyote ile. Lakini nadhani bado tutoe muda kwa serikali ili watuletee taarifa iliyo rasmi zaidi chini ya utaratibu wa kauli za mawaziri kwenye utaratibu wa *order paper* yetu. Nilifikiri hivyo.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kusema machache kuhusiana na hili suala lilioko mbele yetu hapa ambalo limeletwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na kutolewa maelezo na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati. Kama waziri alivyoeleza kwamba suala hili kweli halijajadiliwa ndani ya Baraza la Mapinduzi.

Kutokana na maelekezo ambayo umeyatoa mwenyewe Mhe. Spika, niahidi kwamba tumeyapokea maelekezo hayo na sisi katika kikao kijacho cha Baraza la Mapinduzi tutalizungumza suala hili na baadae tuje tutoe taarifa rasmi katika Baraza lako tukufu. Hatuwezi kuwa na taarifa ya haraka haraka, hatuwezi kusema kitu ambacho hakina kina, lazima tuwe na kitu ambacho tutakieleza kwa kina hapa ili tuweze kuja kufikiria nini chengine cha kukifanya. Kama ulivyosema tuone namna gani Zanzibar inaweza kuathirika kwa kuongeza hizo *mail* za kuongeza eneo la bahari la *EEZ*, vipi Zanzibar tutaathirika au tutanufaika mana inaweza kuwa yote mawili.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunapokea maelekezo hayo na tutayachukua serikali na kuyapeleka katika Baraza la Mapinduzi na baadae tutaleta taarifa rasmi. Nashukuru sana.

Mhe. Spika: Mhe. Ismail Jussa Ladhu serikali imepokea maelekezo hayo ili kuweza kuyafanyia kazi, ahadi ni kwamba kwa kuwa yanahusu kuja kukaa kikao cha Baraza la Mapinduzi jambo hili itabidi lishughulikiwa katika kikao kijacho kama alivyoeleza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, juzi nilipoliibua hili suala katika vyombo vya habari walikusifu kwamba hekima na busara zako zilipelekea suala hili kupata muongozo ulioutoa. Sasa mimi nataka niseme kimsingi sina tatizo kabisa na ombi alilolitoa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais akiwa kiongozi wa shughuli za serikali katika Baraza.

Kwa sababu tu lengo ni jema na nia yote ni kusaidia nchi na watu wake, lakini mimi ningeomba kwa hekima zile zile na busara za Mhe. Spika, kwa lengo la kuisaidia zaidi serikali ili watapojadili katika *cabinet* waweze kupata hisia zetu kwa upanda kuna *concern* mbili tatu, si nia ya kujadili tena taarifa ya Mhe. Waziri aliyoizungumza. Lakini nafikiri tungeutumia huu muda mchache

tulionao ukaturuhusu tutoe zile *concern* zetu kuhusiana na haya ili *cabinet* itapokaa iyazingatie na itakuwa imetutendea haki sisi na imewatendea haki Wazanzibari ambao suala hili limewagusa kiasi kikubwa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningeomba hizi dakika chache tu kabla ya kuahirisha kikao leo Ijumaa saa sita tukapata nafasi ya kueleza *concern* zetu ziko wapi, ili Baraza la Mapinduzi ambacho ndicho chombo kinachosimamia sera za serikali kitapokaa kijue hisia zetu. Kwa sababu lengo sio kuvutana wala kuoneshana ubabae, lengo ni kwamba tusaidiane mwisho vyombo hivi viwili Baraza la Mapinduzi kama ndio chombo cha mamlaka ya utendaji na Baraza la Wawakilishi kama ni chombo cha kusimamia serikali na kutunga sheria viwe vinaelewana katika kulinda kile ambacho tunaamini ni haki na maslahi yetu kama Wazanzibari. Naomba sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kisaidieni kiti tunaonaje?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: mimi nadhani kwa sababu ya maelezo ambayo ameyasema Mhe. Ismail Jussa kusikiliza *concern* za Baraza hiyo haina shida, nadhani tusikilize ili sisi tutakapokwenda kujadili tuyazingatie pia ambayo yametoka kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika: Ki utaratibu ukijadili kitu maana yake una kitu ambacho kiko mezani kilichowasilishwa rasmi kama ni hoja. Kama ingekuwa ni suala la kuuliza maswali iwe suala hasa limekuja rasmi chini ya kauli za mawaziri, sasa kidogo hapa tupaeleze vizuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, umeomba tukisaidie kiti na ninakuelewa kabisa kwamba kutokana na hali yenyewe, naomba nikukumbushe kidogo tu katika busara zako nyingi kikao kilichopita ulitumia kanuni ya 153, mambo yasiyowekewa masharti wakati ule Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alipotutolea taarifa kuhusu ajali ya MV. Spice Islanders, lakini yeye bado ikawa kanuni zimezungumzia kauli za mawaziri na yeye ikawa hatajwi kuwa ni waziri. Ulisema kwamba umetumia mamlaka ya kifungu hiki kumruhusu kusoma taarifa ile. Kwa hivyo, nilikuwa nataka nikuombe kwamba na hili kwa vile halikuwekewa masharti maalum uliruhusu kwa kutumia kanuni hiyo ya 153 Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Sasa tunajadili au tunauliza maswali?

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mimi hoja yangu Mhe. Spika, kwamba kujadili madhali tunazungumza ni kujadili, lakini si kwa lengo la kutoa maelekezo au kutaka kupitisha hoja yoyote hapa. Lakini labda ningesema katika mfumo wa

maswali ambao ningependa serikali iyazingatie ili itapokwenda kukaa katika *cabinet* basi ione kwamba tuna hisia moja, mbili, tatu ili itapokuja kuleta taarifa ilete taarifa nzuri. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Waziri hapa kwamba hili ombi limepelekwa na kwa bahati taarifa alizozitoa yeye mimi bahati mbaya sijaziona kwamba litaamuliwa mwezi wa Julai inawezekana sikusudii kupinga maelezo yake.

Sasa nina hofu kwamba hapo kati kati kwa sababu *process* ikianza baadae kuja kuirejesha inakuja kuwa ni matatizo makubwa. Kwa hivyo, nilikuwa nasema kutokana na uharaka wa suala lenyewe tukaeleza zile hisia zetu ili *cabinet* ikikaa ikazizingatia na itapokuja kutupa taarifa isije ikawa tena tunakuja kutoa maelekezo mengine halafu tena wao wanarudi kutahamaki nenda rudi inakujatukuta tayari tumeshaathirika.

Nasema nirudi katika msingi ule ule kwamba tunaweza kuwa tunalijadili kwa sababu tunalizungumza, lakini lengo likiwa ni kuisaidia serikali kwamba tuna hisia moja, mbili, tatu juu ya suala hili namna lilivyoendeshwa ili baadae serikali iyazingatie hayo kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kuna njia nyingi za kuweza kusaidia jambo hili, tunaweza tukajadili kama jambo la dharura. Lakini shida yangu ni kwamba kuwe kumewasilishwa kitu kiko mezani. Sasa hapa tuna maelezo tu, kama tunakubaliana hivyo ili serikali ipate wasaa wa kujua upeo kiasi gani jambo hili linagusa basi tulipangie siku katika mkutano huu tulijadili hili kam ani jambo la dharura. Nani sasa analeta hoja hiyo, ni serikali au ni Mhe. Jussa uliyetangulia kutoa taarifa hii?

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru tena, nilipoliibua ile juzi utakumbuka kwamba nilitumia kanuni hiyo hiyo ya hoja ya kujadili jambo la dharura. Lakini nikasema kwamba kanuni ilisema kadiri inavyowezekana umtaarifu Spika, lakini kutokana na hali yenyewe ilivyokuwa na ilikuwa ninawasilisha siku ile nilisema hapa. Nilisema kwamba hiyo kadiri inavyowezekana imekuwa haikuwezekana. Sasa kwa sababu ya maelekezo yako mimi ningekuomba utoe busara zako kwa vile serikali ndio inayokwenda kuyafanyia kazi hayo maoni au hisia zetu ambazo zinawakilisha maoni na hisia za wananchi.

Mhe. Spika, mimi kama mtu niliyeleta hoja hii ningeomba uniruhusu niiandae hoja hii kwa ajili ya jambo la dharura na tukijaaliwa Jumatatu niiwasilishe hapa asubuhi, ili tuweze kuijadili na itengeneze muongozo kwa serikali itakapokaa katika *Cabinet* ambayo itawawezesha pia wajumbe kutoa maoni yao

watakapokaa, halafu baadae katika kikao hichi au kikao kinachokuja wakaja wakatuletea taarifa rasmi juu ya suala hili. Ningeomba sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Sina matatizo juu ya hili lakini Jumatatu hii tumeshaipangia kumwambia Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aje amalize mswada. Muda huu tulitaka tuutumie ili usiende bure kwa sababu tukumbuke kwamba kuna siku za mkutano huu tumekubaliana katika Kamati ya Uongozi tutazitumia kwa semina wakati huo kabla ya kujua kama yatatokea haya. Vyenginevyo sasa labda tuseme semina tunaondoa.

Lakini ikija ikichukua muda mrefu hoja hii ya dharura maana yake ni suala la kufanya majumuisho litasogea mbele. Hilo nalo tulione linaweza likaja mpaka siku ya Jumanne na mswada huu nao pia itabidi unasogea mbele huu ambao ulikuwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora auwasilishe.

Isipokuwa labda tuone tu kwamba mjadala huu tuuchukue muda mfupi sana ilimradi ule mswada uje tuumalize kwa ile siku ya Jumatatu hata kama kipindi cha asubuhi pale itakuwa hakitoshi lakini jioni tuumalize ili tupate mtiririko mzuri wa shughuli zetu.

Kwa hiyo, kama ni hivyo basi, nikubaliane na ombi hili la kwamba tayarisha jambo ambalo tulijadili kama dharura kwa kifungu kinachohusika, ili shughuli hizi nyengine ziahirike kidogo tulijadili lile jambo la dharura kuwapa serikali *sentiment* zetu juu ya jambo hili ili walifanyie kazi kwa pamoja hapo baadae.

Basi mara baada ya kipindi cha maswali na majibu siku ya Jumatatu tufanye kazi hii. Mhe. Ismail Jussa Ladhu anachukua hiyo dhamana kwa sababu ndio aliyeleta taarifa ya kuleta hiyo hoja ya dharura. Nafikiri tumefikia pahala.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwa kuwa hoja zinajadiliwa kupitia *order paper* katika kifungu cha 46(1) na (2) cha Shughuli za Kawaida za Baraza. Kwa kuwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametaka kuahirisha hoja yake mpaka Jumatatu. Kwa mujibu wa vifungu hivi haturuhusiki kuingiza shughuli nyengine mpaka ile ikamilike.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba Baraza lako liahirishwe mpaka Jumatatu atakapowasilisha hoja yake.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hii hoja ya mjumbe kama hiyo kanuni tumeiangalia sawa sawa hebu tusomee tena.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, *marginal note* inasema Shughuli za Kawaida za Baraza.

1. Shughuli za Kawaida za Baraza zitatekelezwa kwa njia ya hoja na maagizo mengine yatakayokuwa yamewekwa katika Orodha ya Shughuli.
2. Shughuli za Kawaida zitaanza wakati Spika atakapomwita Mjumbe wa kwanza aliyetoa taarifa ya kuwasilisha mswada au ya kutoa hoja mwanzoni mwa Shughuli za Baraza. Au atamwita Mjumbe anayehusika na hoja ya kwanza iliyo mwanzoni mwa Orodha ya Shughuli na atakapomwita Katibu kusoma Orodha ya Shughuli.

Mhe. Spika: Sasa hii tukiitafsiri ina maana hatuwezi tukaendelea na shughuli hii.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Samahani Mhe. Spika, mpaka ikamilike ya kwanza iliyokuja katika orodha ya *order paper* ndio tena itafuata ya pili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ukisoma kifungu cha 46(1), (2), (3) vyote havisemi kwamba tunaweza tukazuia shughuli mpaka shughuli ya mwanzo iendelee. Kwa hivyo, tunaweza tukafanya shughuli yoyote kama ile imewekwa kwa kipindi chengine. Lakini mimi niungane na Waheshimiwa Wajumbe kwamba kwa hivi sasa nakuomba utumie *wisdom* yako tuliahirishe Baraza hili mpaka hiyo siku ya Jumatatu. Lakini si kwa kifungu hichi cha 46 ni kwa kutumia *wisdom* yako wewe mwenyewe kwa sababu kifungu hichi kinaruhusu kuendelea na shughuli nyengine.

Mhe. Spika: Yaani kifungu hichi kinaruhusu shughuli ziliopo ziendelee ndani ya order paper mpaka ile siku ambayo ilikuwa tufanye shughuli ya dharura ili tuiahirishe halafu imalizike ile tuendelee na shughuli zetu za kawaida. Nafikiri hiyo ndio tulikuwa tunafanya hata wakati wa Bajeti, likitokea jambo la dharura tunazuia suala la bajeti kidogo likimalizika lile tunaendelea na bajeti yetu. Nadhani ndivyo ilivyokuwa.

Lakini hoja ya Mhe. Mjumbe kwamba basi nitumie mamlaka ya kusitisha shughuli mpaka Jumatatu ili tuone tunakuja kufanya shughuli ya dharura baada ya hapo tumalize shughuli ya waziri na hatimae twende na mswada wa rushwa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, mimi Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alivyowasilisha hoja yake na ametumia kifungu cha kanuni kwamba hoja hii iahirishwe kwa muda wa masaa 6 ili apate nafasi ya kuyapitia na wala hakusema siku ya Jumatatu. Kwa hivyo, naomba

suala la kujibu hoja iliyowasilishwa na Mhe. Waziri izingatiwe kwamba kaomba iahirishwe kwa muda wa masaa 6 nawe Mhe. Spika ukakubaliana na hilo kulingana na mazingira yenyewe. Kwa hivyo, hoja izingatiwe ambayo Mhe. Waziri ameiwasilisha. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Naona hilo tulilimaliza baada ya ombi alilotoa nikasema ombi hilo nalikubali ili kutoa muda wa kutosha lifanyike Jumatatu. Sasa kwa sababu ya jambo la dharura ambayo inakubalika ndani ya kanuni zetu hizi tukasema hiyo siku ya Jumatatu mara tu baada ya kipindi cha maswali lije suala hili ambalo Mhe. Ismail Jussa Ladhu atalisema kwa sababu ya neno dharura na kanuni zetu ndio zinaruhusu hivyo.

Sasa baada ya ile shughuli ya dharura tuje kumaliza hoja ya mheshimiwa ambapo atafanya majumuisho na baadae ndipo sasa tuje na Mswada wa Rushwa. Hivyo ndivyo ambavyo mtiririko na hasa baada ya maombi aliyoyasema Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na nilipoangalia muda ya wajumbe inaonekana wako tayari kuweza kuahirisha shughuli hii mpaka siku ya Jumatatu. Kazi ya kwanza siku hiyo ya Jumatatu itakuwa ni ya shughuli ya dharura baadae tunamalizia Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kisiasa na baadae tunakwenda na mtiririko wa mswada kuhusu rushwa.

Kwa hivyo, nafikiri tukubaliane hivyo na nakubali mashauri hayo na naomba sasa tusitishe shughuli zetu hadi siku ya Jumatatu tarehe 23/01/2012 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 5:40 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 23/01/2012 saa 3:00 asubuhi)